



# UBORA WA MAUDHUI YA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA

# 2019





**IMETAYARISHWA NA:**

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na  
Mawasiliano kwa Umma  
S.L.P 4067 Mikocheni B  
Makaburi Street, Plot Block D, No.34  
Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255 22 2700756  
Barua pepe: sjmc@udsm.ac.tz

# UBORA WA MAUDHUI YA VYOMBO VYA HABARI TANZANIA

**WATAFITI**

Abdallah Katunzi  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma

Christoph Spurk,  
Zurich University of Applied Sciences, Institute of Applied  
Media Studies

**MFA SIRI**

Dkt. Gidion Kamfipo  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma

**WASANIFU**

Essy Ogunde  
@Creative Press Ltd

Nuzulack J. Dausen  
@Nukta Africa

Haki zote zimehifadhiwa.

## Yaliyomo

SHUKRANI.....	02
UFUPISHO.....	03
1.0 UTANGULIZI.....	04
2.0 UKTADHA WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI TANZANIA .....	05
3.0 MBINU ZA UTAFIGI .....	09
4.0 MATOKEO .....	12
5.0 UBORA WA MAUDHUI NA MTAZAMO WA WADAU .....	40
6.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	42
VIAMBATANISHO.....	44

## Shukrani

---

Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) inatoa shukrani za dhati kwa Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania kwa kufadhili utafiti huu **“Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania 2019”**, na kwa jitihada zao endelevu za kuinua ubora wa vyombo vya habari na taaluma ya Uandishi wa Habari nchini.

Tunathamini na kushukuru wadau wa habari kwa utayari wao endelevu na kuunga mkono jitihada hizi zinazolenga kutafti ubora wa maudhui ya vyombo vya habari nchini. Maoni yao kwenye warsha ya wadau iliyolenga kupitia upya vigezo vya ubora wa maudhui, utayari wao kusaidia wakati wa kurekodi kazi za kihabari na uwazi wao wakati wa mahojiano ni ishara tosha ya mchango wao uliotukuka katika kuunga mkono jitihada za kuimarisha ubora wa vyombo vya habari nchini.

Zaidi ya hapo, shukrani zetu za dhati zinaenda kwa Prof. Michael Andindilile wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Prof. George Nyabuga kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuipitia kazi hii. Hakika mchango wao ni wa thamani kubwa.

Tunawiwa kuwashukuru watafti wasaidizi kwa namna walivyojitoa kwenye tafiti hii: Dkt. Joyce Bazira, Shekha Ally Hussein, Swaum Manengelo, Sebastian Okiki, Dianus Ishengoma, Vaileth Barden, Theodora Munisi, Theodora Theodory, Casiana Mwanyika, Faidha Ngaga, Pascael George, Nehemiah Mihayo, Angela Mondi, Safina Yasini, Amina Lweno, Masekepa Asangama, Ally Bakari, Amani Goodhope, Carlos Banda, Thobias Masalu, Aisha Makame, Suleiman Chombo, Goodluck Paul, Khalila Abdul Shaban, Shadida Salum, na Venance Majula.

## Ufupisho

Kwa ujumla, mwaka 2019 ubora wa uripoti kwa vyombo vya habari nchini ulishuka ikilinganishwa na mwaka 2018. Kielezo cha Ubora kwa vyombo vyote vya habari kilishuka hadi asilimia 26.8 ikilinganishwa na asilimia 28 za mwaka 2018. Kwa mwaka 2019 magazeti yameporomoka zaidi katika ubora wake.

Kwa sasa vyombo vya habari hutumia zaidi vyanzo vichache vya habari ikilinganishwa na mwaka 2018. Uwingi wa vyanzo vya habari umeshuka kwa asilimia 5. Kinachotisha zaidi na zaidi watoa habari hawako tayari kuelezea maoni yao halisi, jambo hili linathibitishwa na ripoti hii kwenye kiashiria kinachochunguza "idadi ya mitazamo na maoni" kama ambavyo yameelezwa na wanahabari ikiwa imepungua ikilinganishwa na mwaka 2018. Na ujumuishi wa maoni kinzani kwenye kazi za kiuandishi kama kipengele muhimu cha kuibua mjadala kwenye jamii kimeshuka kama ilivyoshuka idadi ya maoni yenye kukosoa serikali. Hii inaonyesha kikwazo kikubwa kwa jamii kwa mwaka 2019. Kwa wastani, ni asilimia 2.8 tu ya habari ndizo zilitoa mitazamo kinzani.

Zaidi ya hapo, ikilinganishwa na mwaka 2018, uripoti wa vyombo vya habari umekuwa wa juu juu zaidi kwani habari nyingi kwenye magazeti, redio na televisheni hazioneshi kwa kina mtazamo ambao kwao mada ya habari au kipindi hicho kimezingatia. Ni taarifa za wazi na za juu juu tu ndizo zinazotolewa pasipo kuripoti mada husika kwa kina zaidi, ikiangazia kwa mfano matokeo yake kiuchumi, kisheria au kisiasa n.k. Kiashiria cha Ubora kinachohusu ujumuishwaji wa "idadi ya mitazamo" kimeshuka kwa asilimia 11 kwa kila makala au habari iliyoripotiwa.

Hata hivyo kuna maboresho machache kwa mwaka 2019. Habari zinazojumuisha kiini cha habari au sababu za msingi za kutokea tukio husika zimeongezeka kwa mwaka 2019. Vile vile kwa sasa kuna ongezeko la habari zinazoweka takwimu dhahania kwenye muktadha ili kuzifanya takwimu hizo kueleweka vizuri. Pia, kuna maboresho kidogo kwenye vyombo vya habari ambapo vimekuwa vikitegemea zaidi jitihada za binafsi kutafuta habari zao na kwa namna fulani vimepunguza uripoti unaotegemea habari za matukio kama mikutano na waandishi wa habari

(press conferences), warsha, uzinduzi nk. kutoka asilimia 60 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 58 mwaka 2019.

Katika jitihada za kubainisha sababu za hali hii ya ubora wa maudhui kwa vyombo vya habari, mahojiano yaliyofanyika na wadau wa habari wakiwamo wahariri yanaonesha kwa sasa kuna changamoto kubwa tatu zinazozikabili vyombo vya habari. Wadau hao wanaona kwamba mazingira ya sasa ya kisiasa ni kikwazo kwa uhuru wa habari nchini huku ikishuhudiwa baadhi ya vyombo vya habari vikifungiwa kwa muda mfupi au mrefu sana kujishughulisha na mambo ya habari. Hali hii imepelekea udhibiti binafsi ndani na nje ya vyombo vya habari. Katika mazingira haya hata baadhi ya vyanzo vya habari huogopa kuzungumza na vyombo vya habari.

Changamoto nyingine ni ile inayohusiana na ugumu wa mazingira ya kiuchumi. Mapato yatokanayo na matangazo yamepungua huku hadhira ikihamia kwenye vyombo vya habari vya kidijitali. Hali hii imesababisha baadhi ya vyombo vya habari kupunguza wafanyakazi huku vingine vikishindwa kulipa wafanyakazi wao mishahara. Vingine vinajipapatua visiende na maji.

Changamoto ya tatu ni ile inayohusiana na viwango vya kiweledi. Kwa nyakati fulani wahariri hawawezi au hawako tayari kuzingatia viwango vya kiweledi. Baadhi ya vyombo vya habari sio tu husimamiwa na wahariri wasio na uzoefu bali pia huajili waandishi wasio na vigezo.

Changamoto hizi tatu kama zilivyofafanuliwa hapo juu - za kisiasa, za kiuchumi na za kwenye vyumba vya habari - bila shaka zimechangia kuporomoka kwa viwango na hali ya uripoti wa vyombo vya habari nchini.

## 1.0 UTANGULIZI

---

Tasnia ya habari nchini imekua mno tangu mapinduzi yake ya kiliberali miaka ya 1980 na 1990. Hata hivyo, ingawa tasnia imekuwa inakua kwa idadi, hapajafanyika utafiti katika ngazi ya kitaifa kuelewa ubora ya tasnia zaidi ya ule wa uliohusu *Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania 2018*. Ripoti hii inayohusu *Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania 2019* ni mwendelezo wa jitihada zilizoanzishwa mwaka 2018 ikiendelea kuchunguza zaidi ubora wa uripoti wa vyombo vya habari nchini.

Mahsusi kabisa inachunguza utendaji katika uripoti wa vyombo vya habari ikitumia viashiria vya ubora vilivyokubalika na wadau wa habari ikijumuisha vyumba vya habari, mashirika ya kitaifa ya vyombo vya habari visivyokuwa vya kiserikali, mashirika ya kimataifa ya habari yanayofanya kazi nchini, mashirika yanayosimamia weledi katika sekta ya habari, wanataaluma na wawakilishi toka serikalini.

Ripoti hii ina sehemu sita nne ambazo ni; Utangulizi; Muktadha wa vyombo vya habari nchini Tanzania; Mbinu za utafiti; Matokeo (kwa idadi na kwa ubora); Maoni ya wadau; na hitimisho na mapendekezo. Uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwenye ripoti hii umejiegemeza kwenye vigezo vya kiubora ikianza na kutoa matokeo ya jumla kwa vyombo vyote vya habari kabla ya kuvitenga katika tanzu zake kama vile vyombo vya habari vya uchapishaji, redio na Televisheni. Muhtasari wa matokeo kwa kila chombo cha habari unatarajiwa kuwekwa kwenye tovuti ya UDSM-SJMC (<https://www.udsm.ac.tz/web/index.php/schools/sjmc>) ukiingia kupitia menyu ya *Yearbook on Media Quality in Tanzania*.

## 2.0 MUKTADHA WA VYOMBO VYA HABARI NCHINI TANZANIA

Mapinduzi ya vyombo vya habari yaliyofanyika kuelekea mwishoni mwa miaka ya 1980 ndiyo yaliyoashiria mwanzo wa kupanuka kwa vyombo vya habari nchini. Gazeti la Business Times (Gazeti la kwanza la kila wiki) lilichapishwa mwaka 1988; *Majira* (Gazeti la binafsi la kwanza la kila siku) lilionekana kwenye meza za kuuzia magazeti mwaka 1993; *Radio One* (Stesheni ya redio ya kwanza ya binafsi) ilianza kurusha matangazo yake mwaka 1994, na *Coastal Television Network* (CTN) (Kituo cha kwanza cha televisheni) kilienda hewani mwaka 1994 (ibid.). Ni muhimu kukumbukwa kwamba stesheni ya televisheni ya kwanza ya rangi ilizinduliwa mwaka 1974 kule Zanzibar.

Hadi kufikia mwezi Machi 2020 kulikuwa na vituo vya redio 183 (ongezeko kubwa ikilinganishwa na vituo 98 vilivyokuwepo mwaka 2014), vyombo vya huduma ya utangazaji 43<sup>1</sup> (ikilinganishwa na 36 mwaka 2014),<sup>2</sup> magazeti na majarida 229 (ikilinganishwa na 216 yaliyokuwepo mwaka 2018).<sup>3</sup> Hadi kufikia mwaka 2016, kulikuwa na vituo 25 vya redio na vituo 12 vya televisheni visiwani Zanzibar. Mwaka 2016, Tume ya Utangazaji Zanzibar ilipokea maombi matatu ya vituo vipya vya redio; hata hivyo maombi hayo hayakushughulikiwa kwa kukosa nafasi kwenye masafa yaliyotengwa. Zanzibar ilikuwa imepewa MHz 25 tu na Shirika la Mawasiliano la Kimataifa (ITU) na ilikuwa imeshazitumia zote. Matokeo yake, maombi mapya kwa ajili ya redio mpya yameshauriwa kuelekezwa kwa watoa huduma wa ndani (Multiplex operators) ambao wanaweza wakawapa masafa.<sup>4</sup>

Ukiachana na ukuaji wa vyombo vya habari vya asili (magazeti, redio na TV), nchi inashuhudia mabadiliko ya kimwelekeo kwenye uga wa intaneti. Kwa kipindi cha miaka saba iliyopita ueneaji wa matumizi ya intaneti umeongezeka kutoka asilimia 17 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 46 mwaka 2019. Hadi kufikia mwezi Machi 2019, takribani watanzania 25,794,560 (ongezeko zaidi kutoka 23,142,960 mwaka 2018)<sup>5</sup> walikuwa wakitumia intaneti, huku wengi wao wakipata intaneti kupitia mfumo jongefu usiotumia nyaya (mobile wireless). Mabadiliko haya japo yanaonekana kutokea

zaidi mijini yanatoa fursa kwa raia kupata habari za mitandaoni kupitia vifaa vyao vya kielekroniki huku wakishiriki mijadala ya kijamii na kuchochea uandishi wa habari wa kiraia (citizen journalism).

### 2.1 Mazingira ya kisheria na uhuru wa habari

Kuna utitiri wa sheria zinazosimamia utendaji wa tasnia ya uandishi wa habari nchini. Zinazofahamika zaidi ni Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na Kanuni za Mawasiliano ya Kimtandao na Posta (maudhui ya kimtandao) za mwaka 2018. Sheria ya Huduma za Habari inaeteleza uundwaji wa vyombo mbalimbali ikiwamo Bodi ya Usimamizi na Utoaji leseni kwa Waandishi (*Journalists Accreditation Board*), Baraza Huru la Habari, na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari.

Hata hivyo vyombo hivi bado havijaanzishwa. Kupitia kanuni zake za mwaka 2017, Sheria hii inaweka Stashahada ya Uandishi wa Habari kama kiwango cha chini kitaaluma na kiweledi kitakachomuwezesha mwanahabari kufanya kazi za uandishi wa habari nchini huku serikali ikitoa muda wa miaka mitano hadi 2021 kwa ambao hawana kiwango hicho cha elimu kujiendeleza na kukifikia. Mpaka sasa, hakuna taarifa za wazi kitaifa zinazoonesha ni kwa kiasi gani waandishi wamejiendeleza kielimu ili kutimiza hitaji hilo la msingi la kisheria.

1. TV stations, satellite TV, Digital Terrestrial Television (DTT), and Digital to Home (DTH)

2. <https://www.tcra.go.tz/publication-and-statistics/statistics>, Machi 2020

3. <http://www.maelezo.go.tz/>, takwimu za haraka

4. MCT State of the Media in Tanzania 2016

5. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), idadi ya watu kwa mwaka 2018 ilikadiriwa kuwa 54,199,163.

Utafiti wa 2019 kwa vituo 40 vya redio nchini uliofanywa na Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) kama sehemu ya Mradi wa UNESCO wa mafunzo kwa njia ya mtandao ulibainisha kwamba waandishi wa habari 192 (asilimia 55) kati ya waliohusishwa kwenye utafiti huo walikuwa hawana Stashahada ya Uandishi wa Habari.

Kwa kuhofia matokeo ya changamoto hii na athari zake kwa vituo vya redio, UNESCO ikishirikiana na Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) waliamua kuikabili changamoto hii kwa kuanzisha masomo kwa njia ya mtandao ili kuwawezesha waandishi wa habari walioko kazini hasa walioko kwenye vituo vya redio vya ndani kujiandikisha na kusoma kozi hiyo kwa njia ya mtandao. Masomo kwa wanafunzi wa awamu ya kwanza yameanza mwaka huu 2020.

Kuhusiana na mazingira ya kisheria yaliyopo, bado kuna maswali mengi kuhusiana na uhuru wa vyombo vya habari nchini. Mwaka 2019 gazeti la *The Citizen* lilizuiliwa kuchapishwa kwa siku saba kwa kile Msajili wa Magazeti alichokiita kuandika kwa makusudi habari za upotoshaji kuhusu thamani ya shilingi ya Tanzania pasipo kuwasiliana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).<sup>6</sup>

Hata hivyo inapaswa kukumbukwa kwamba miaka ya nyuma, kwa sababu mbalimbali, magazeti yalikuwa yanafungwa au kuzuiliwa kuchapishwa kwa vipindi mbalimbali kuanzia miezi mitatu hadi miaka mitatu. Mwaka 2017,<sup>7</sup> gazeti la *Tanzania Daima* lilizuiliwa kuchapishwa kwa siku 90; Mwaka 2017,<sup>8</sup> *Raia Mwema* lilifungwa kwa miezi mitatu, *Mawio* lilifungwa kwa miaka miwili mwaka 2017,<sup>9</sup> *Mwanahalisi* lilifungwa kwa miaka miwili mwaka 2017.<sup>10</sup> Mwaka 2016<sup>11</sup> *Mseto* lilifungwa kwa miaka mitatu. Kwa ujumla, mwaka 2017 unaonekana kuwa mwaka mchungu zaidi kwa uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania.<sup>12</sup>

Zaidi ya hapo, serikali kwa kutumia Kanuni za Mawasiliano ya Kimtandao na Posta (maudhui ya kimtandao) imevisimamia vilivyo vyombo vya habari vya mtandaoni na imeweka ulazima wa kisheria kwa vyombo vyote vinavyorusha maudhui ya kimtandao kujisajili TCRA. Hadi kufikia Novemba 12, 2018, TCRA ilikuwa

imeshatoa leseni<sup>13</sup> 224 kwa watoa huduma za kimaudhui mtandaoni.

Mwezi Septemba 2019, televisheni mbili za mtandaoni - *Millard Ayo TV na Watetezi TV* - kila moja ilipigwa faini ya shilingi za kitanzania milioni 5 (Takribani dola 4,350 za kimarekani) na TCRA kupitia Kamati yake ya Maudhui kwa kushindwa kuchapisha sera zinazoongoza vyombo vyao vya habari na kanuni za mlaji (*User Charters*). Televisheni nyingine ya mtandaoni, *Kwanza TV*, ilifungwa kwa miezi 6 kwa kile kilichoelezwa kuchapisha habari za uongo za zenye kupotosha kwa mujibu wa kanuni za maudhui ya mtandaoni.<sup>14</sup>

*Watetezi TV*, inayomilikiwa na Shirikisho la Watetezi wa Haki za Binadamu nchini (*Tanzania Human Rights Defenders Coalition* (THRDC)) ilikata rufaa Tume ya Ushindani (*Fair Competition Tribunal* (FCT)) dhidi ya maamuzi ya Kamati ya Maudhui ya TCRA. Kwenye hukumu yake FCT iliamua kwamba kwa mujibu ya kifungu cha 18 cha kanuni za maudhui ya kimtandao, Kamati ya Maudhui haikuwa na mamlaka ya kutoza faini. Ilongeza kwamba kifungu cha 18 kitatumika ikiwa tu kuna hukumu ya mahakama. Hata hivyo, FCT iliipunguzia faini *Watetezi TV* kutoka shilingi milioni 5 (takribani dola za Kimarekani 2,200) hadi shilingi milioni 3 (takribani dola 1,300 za Kimarekani).

Utafutaji wa haki mahakamani (*Litigation*) ndiyo inayoonekana kuwa njia inayokubalika miongoni mwa wadau wa habari katika kutatua masuala yanayohusiana na uhuru wa habari. Mwezi Juni mwaka 2018, Mahakama ya Afrika Mashariki iliagiza serikali kuondoa zuio lake kwa gazeti la *Mseto*.<sup>15</sup> Mwaka 2015, Mahakama Kuu ya Tanzania iliondoa zuio lililokuwa limetolewa mwezi Julai mwaka 2012 kwa gazeti la *Mwanahalisi*.<sup>16</sup>

<sup>6</sup> <https://www.theeastafrican.co.ke/news/ea/Tanzania-suspends-newspaper-over-story-on-falling-shilling/4552908-5002264-r1s0fdz/index.html>

<sup>7</sup> <https://www.thecitizen.co.tz/News/Govt-bans-Tanzania-Daima-newspaper-for-90-days/1840340-4154086-lilil03/index.html>, retrieved on 15th December 2018

<sup>8</sup> <http://www.africanews.com/2017/09/29/another-tanzanian-newspaper-banned-for-criticizing-the-government/>, retrieved on 15th December 2018.

<sup>9</sup> <https://qz.com/africa/1009353/magufulis-government-has-shut-tanzanian-newspaper-mawio-for-two-years/>, retrieved on 20th December 2018

<sup>10</sup> <https://www.thecitizen.co.tz/News/Govt-bans-Mwanahalisi-for-two-years/1840340-4102400-oyh5nc/index.html>, retrieved on 15th December 2018

<sup>11</sup> <https://www.theeastafrican.co.ke/news/ea/Tanzaniabans-Mseto-newspaper-for-three-years/4552908-3340844-rfjjcz/index.html>

<sup>12</sup> MCT's Media Watch, September 2018, page 7

<sup>13</sup> <https://www.tcra.go.tz/licensed-online-content-services-providers>

<sup>14</sup> <https://rsf.org/en/news/tanzania-slaps-harsh-sanctions-three-online-tv-channels>

<sup>15</sup> <https://www.article19.org/resources/tanzania-ea-court-ruling-upholds-media-freedom-in-reversing-newspaper-ban/>

<sup>16</sup> The newspaper is no stranger to closures. In 2008, it was banned for three months; in 2012, for two years; and in 2017, for two years.



Hukumu hizi zinaonesha kwamba bado kuna njia mbadala ambazo wanahabari na wadau wa habari wanaweza kuzitumia ili kukabiliana dhidi ya matumizi yasiyo ya kiungwana ya sheria yanayofanywa na mamlaka za kiserikali na matumizi mabaya ya madaraka.

Maelezo yaliyotolewa hapo juu yanaonesha kuporomoka kwa uhuru wa habari nchini. Viashiria vya Uhuru wa Habari vilivyochapishwa na Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka (*Reporters without Borders*) vinaonesha hali ya kutisha ya kuporomoka kwa uhuru wa habari nchini. Mwaka 2016, nchi iliwekwa kwenye nafasi ya 71<sup>17</sup> (kati ya nchi 180), mwaka 2017,<sup>18</sup> nafasi ya 83, nafasi ya 93 mwaka 2018,<sup>19</sup> nafasi ya 118 mwaka 2019, na nafasi ya 124 mwaka 2020, ikiwa imeporomoka kwa nafasi 53 tangu mwaka 2016.

## 2.2 Mazingira ya Biashara ya Vyombo vya Habari

Mazingira ya biashara ya vyombo vya habari yameendelea kuonesha kushuka kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara, kuhama kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara kutoka kwenye vyombo vya habari vya asili kwenda kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni huku pia hadhira ikihama kutoka vyombo vya habari vya asili na kuhamia vya mtandaoni.

Kushuka kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara yanayokadiriwa kuwa kati ya asilimia 50 na asilimia 70,<sup>20</sup> yanahusishwa na maamuzi ya serikali kubana matumizi kwa kupunguza bajeti ya matangazo, maamuzi ya sekta binafsi ya kupunguza fungu lake katika bajeti za matangazo na kujitangaza ikiwa ni matokeo ya hali ngumu ya kiuchumi ilivyo sasa.<sup>21</sup> Kushuka huko pia kunahusishwa na maamuzi ya watoa matangazo wakubwa walioamua kutangaza kwa bei nafuu kupitia mitandaoni. Hali hii haikubadilika mwaka 2019.

Pasipo kupuza nia njema ya serikali katika kubana matumizi yake, palikuwa na mtazamo ulioaminika "miongoni mwa waandishi wa habari, wahariri na wachambuzi kwenye vyombo vya habari kwamba serikali ambayo imekuwa ndiye mtoa matangazo mkuu kwa vyombo vingi vya habari nchini, ilikuwa ikipendelea katika utoaji wa matangazo ikivipendelea zaidi vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali huku ikiyanyima

matangazo muhimu magazeti binafsi hasa yaliyodhaniwa kuegemea kuviunga mkono vyama vya siasa vya upinzani au baadhi ya viongozi wa upinzani". Maamuzi ya serikali kuyanyima matangazo baadhi ya magazeti yamekuwa yakiendelea kwa miaka mingi na mara nyingi wahanga wakuu ni vyombo vya habari vinavyochapisha au kutangaza habari ambazo zinakosoa mamlaka za kiserikali.<sup>22</sup>

Kupungua kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara kumeathiri mno biashara ya vyombo vya habari nchini. Mwezi Oktoba mwaka 2019,<sup>23</sup> redio inayoendeshwa kibiashara ya *Lake FM* inayopatikana Mwanza ilifungiwa na TCRA kwa kushindwa kulipia tozo za masafa na za kiusimamizi. Kwa redio inayojiendesha kibiashara kufungiwa kwa kushindwa kulipa tozo ni ishara inayoonesha ni kwa namna gani mazingira ya biashara ya vyombo vya habari nchini yalivyo na changamoto. Redio hiyo iliendelea na shughuli zake mwezi Januari mwaka 2020.

Licha ya kushuka kwa mapato yatokanayo na matangazo ya biashara sambamba na kupungua kwa hadhira, kuna jitihada za dhati zilizochochuliwa na vyombo vya habari vya asili (legacy media) kuongeza aina za vyanzo vyao vya mapato kwa kutengeneza njia nyingine mpya za kujipatia kipato kutokana na matangazo ya biashara na kutengeneza "maudhui pendwa" yatakayovutia hadhira kubwa zaidi.

Mwaka 2018, kampuni ya Mwananchi Communications Limited (MCL), wachapishaji wa magazeti ya *Mwananchi*, *The Citizen* na *Mwanaspoti*, ilianzisha jukwaa lililoitwa *Jukwaa la Fikra*. Licha ya kutoa nafasi kwa mijadala ya wazi kuhusu masuala mbalimbali yanayoiathiri jamii kufanyika hapo, jukwaa hilo pia hutumika kama njia ya ziada ya kujiongezea kipato kwani imekuwa ikiwavutia wadhamini na watoa matangazo ya kibiashara. Tangu kuanzishwa kwake, MCL imeendesha jukwaa hilo mara 5.<sup>24</sup>

<sup>17</sup> <https://rsf.org/en/ranking/2016>

<sup>18</sup> <https://rsf.org/en/ranking/2017>

<sup>19</sup> <https://rsf.org/en/ranking/2018>

<sup>20</sup> Mahojiano ya wahariri

<sup>21</sup> MCT State of the Media in Tanzania 2016

<sup>22</sup> MCT State of the Media in Tanzania 2016

<sup>23</sup> Awali kituo hiki cha redio kilijumuishwa kwenye sampuli ya utafiti huu, lakini kilitolewa baada ya huduma zake kusitishwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

<sup>24</sup> <https://mcl.co.tz/mwananchi-thought-leadership-forum-mtlf-v/>

Kampuni ya magazeti inayomilikiwa na serikali (Tanzania Standard Newspapers (TSN)), vile vile huandaa majukwaa ya kibiashara ya mikoa ili kuinua shughuli za kitaifa za kijamii na kiuchumi zinazoendelea ndani na nje ya nchi. Japokuwa majukwaa hayo huandaliwa kwa lengo la kuchochea uwekezaji mikoani, pia yamekuwa yakivutia wadhamini na hivyo kuchangia kama chanzo cha mapato. TSN pia inatoa huduma mbalimbali kama vile kutengeneza makala, tafsiri n.k.

Shirika la Utangazaji Tanzania (Tanzania Broadcasting Corporation (TBC)) ambalo humilikiwa na serikali kupitia chaneli yao ya televisheni (TBC1) ilijipanga upya kibiashara kwenye kipindi chake cha taarifa ya habari kwa kuanzisha utamaduni mpya wa studio - mwonekano tofauti wa studio, watangazaji na mtindo wa utangazaji. Maboresho hayo yamelenga kutengeneza usawa kati ya mtindo wa utangazaji na kile kinachotangazwa kwenye taarifa ya habari ikifahamika kama *Aridhio*. Maboresho haya pia yamelenga kuongeza watazamaji na mapato yake.

Jitihada zingine zinajumuisha uhamaji kutoka matangazo ya biashara ya moja kwa moja kuelekea matangazo ya kibiashara-habari (*advertorials*), kupunguza gharama za matangazo, kuanzishwa kwa vyombo vya habari vya mitandaoni ili kukamata fursa ya matangazo ya mitandaoni na hadhira ya mtandaoni, kutoa huduma za uchapishaji kwa vyombo vingine vya habari, kupanua wigo wa aina za biashara ikiwamo kuanzisha huduma za usafirishaji wa vifurushi na mizigo (*courier services*), n.k. Bado haijafahamika kama mawazo<sup>26</sup> haya mapya yanaweza kuzalisha mapato mapya na kuongeza ukubwa wa hadhira. Hata hivyo ni suala linalohitaji kufuatiliwa kwa ukaribu.

Vile vile, kuongezeka kwa hadhira ya mtandaoni kumeathiri mauzo ya magazeti. Ingawa hakuna takwimu za kitaifa kuhusu mauzo ya magazeti, wahariri wanathibitisha kwamba takwimu za mauzo zimekuwa zikishuka kwa kasi mno. Hili hutokana na ukweli kwamba watu wanaweza kupata habari mitandaoni bure kabisa. Hata hivyo, kushuka kwa takwimu kumeyalazimisha magazeti kuhamishia maudhui yao mitandaoni ikiwa ni jitihada za kuendelea kuishikilia hadhira yao ya sasa na kuvutia hadhira mpya.

Kwa hiyo vyumba vya habari vinahitaji kuwekeza

nguvu katika mikakati endelevu. Mikakati hiyo ya baadae lazima ilenge kufikia malengo matatu. Mosi, kupanua wigo wa vyanzo vya mapato; pili kuanzisha mkakati wa kuhamia mtandaoni ili kupata hadhira na watoa matangazo ya mtandaoni; na tatu, kuendesha kampeni kutaka mazingira rafiki ya kisheria kwa vyombo vya habari.

Kando ya usuli huu, uchunguzi huu wa ubora wa uripoti wa vyombo vya habari unaweza kuwa sehemu ya suluhisho kwa maendeleo ya baadae ya vyombo vya habari nchini kwani uripoti bora unaweza kuongeza hadhira na kuvutia matangazo zaidi ya kibiashara. Hatimaye hili litaletela ongezeko la mapato na ongezeko la vyanzo vikubwa vya mapato.

### 3.0 MBINU ZA UTAFITI

Ili kuchunguza ubora wa uripoti wa vyombo vya habari, tafiti hii imetumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui (*content analysis*) kama njia fanisi fanikishi na isiyo na upande ya uchambuzi wa ripoti za kihabari (habari, makala, vipindi n.k.) kulingana na vigezo mahsusi vikitumika pamoja na hojaji za kina.

#### 3.1 Vigezo vya ubora

Utafiti huu hutumia neno “Ubora” kama muhtasari wa dhana pana inayobeba vigezo vya ubora kwani ubora kama ubora si rahisi kupimika. Badala yake, ni rahisi kupima kwa kuzingatia vigezo mbalimbali bainifu vya ubora ambavyo ni vipengele tofauti tofauti vya ubora wa jumla.

Vigezo vya ubora vinavyotumika katika utafiti huu vimeegemea katika nadharia ya uandishi wa habari. Pande zote mbili yaani wanataaluma na waandishi walioko kazini wamekubaliana kuvitambua vigezo husika vya ubora ambavyo viliandaliwa kutoka kwenye mabadilishano ya mawazo na warsha zilizowahusisha wahariri, waandishi wa habari, wanablogu, na wengineo. Vigezo vya ubora huangalia vipengele tofauti vya uandishi wa habari, zaidi zaidi kuhusu:

- a. Weledi katika kazi ya Uandishi wa Habari
- b. Utoaji wa taarifa toshelevu kwa hadhira lengwa
- c. Uelewekaji wa habari kwa hadhira; na
- d. Maadili ya Uandishi wa Habari

## Jedwali 1: Vigezo vikuu vya ubora

Kipengele cha Uandishi wa habari	Vigezo vya ubora - nini kinapaswa kuangaliwa
Weledi	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuripoti kunakozingatia vyanzo vingi vya habari kutoka makundi mbali mbali ya kijamii.</li> <li>Kuripoti habari za matukio au kutafuta habari kwa jitihada binafsi.</li> </ul>
Utoaji wa taarifa kwa kina	<ul style="list-style-type: none"> <li>Uripoti unaozingatia mitazamo mbalimbali</li> <li>Uripoti unaoelezea kiini cha tukio/suala/tatizo</li> <li>Uripoti unaozingatia usuli wa kihistoria wa tukio/suala/tatizo</li> <li>Kutoa maoni na mitazamo mbalimbali kuhusiana na tukio/suala/tatizo</li> <li>Kutoa maoni kinzani na yenye usawa.</li> </ul>
Kueleweka kwa habari na hadhira	<ul style="list-style-type: none"> <li>Habari iko vizuri</li> <li>Mpangilio wa habari umekaa vizuri (mtiririko, muunganiko wa mantiki)</li> <li>Matumizi ya takwimu katika muktadha bora</li> </ul>
Maadili	<ul style="list-style-type: none"> <li>Haki ya kujibu inapaswa kutolewa (ikiwa kuna tuhuma dhidi ya watu au taasisi)</li> </ul>

Kutimizwa kwa vigezo hivyo vya ubora ni jambo muhimu mno katika kipindi hiki wakati uandishi wa habari wa kiraia unakua. Kwa hiyo, aina zote za vyombo vya habari (vya uchapishaji, redio na televisheni) vinatakiwa kuongeza kitu fulani chenye upekee kwenye uripoti wa tukio, kitu ambacho hadhira itakithamini. Nyongeza hiyo ya thamani kwenye uripoti itachangia kueleweka vizuri kwa hadhira.

### 3.2 Sampuli ya vyombo vya habari

Vyombo vingi zaidi vya habari vilijumuishwa katika mradi huu ikilinganishwa na mwaka 2018 na 2017. Kulikuwa na vyombo vya habari vilivyoshiriki kwenye mradi huu kwa mara ya kwanza kama vile *Habari Leo*, *Raia Mwema*, *Mwanahalisi Online*, *ZBC TV*, na *Safari FM*.<sup>25</sup>

Katika ujumla wake, vyombo vya habari 29 vilichaguliwa kushiriki kwenye utafiti huu wa mwaka 2019 ikijumuisha magazeti kumi (10), redio tano (5) za kitaifa, redio nane (8) za mikoani, vituo vitano (5) vya televisheni na jukwaa moja (1). Uchaguzi huu wa vyombo vya habari una uwakilishi wa aina zote za vyombo vya habari: Vya umma, vya binafsi, vyenye masafa yanayotandaa nchi nzima au zile za mikoani na vyombo vya habari vya mtandaoni.

<sup>25</sup> Kwanza TV na Lake FM zilichaguliwa kuingia katika utafiti huu, lakini zilitolewa baada ya huduma zao kusitishwa kwa muda na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

## Jedwali 2: Sampuli ya vyombo vya habari

Magazeti		Redio za kitaifa		Redio za kijamii		Televisheni		Jukwaa
<i>The Citizen</i>	77	<i>TBC Taifa</i>	80	<i>Pangani FM</i>	65	<i>TBC1</i>	56	<i>Jamii Forums</i>
<i>Daily News</i>	79	<i>Radio Free Africa</i>	64	<i>Dodoma FM</i>	59	<i>ITV</i>	63	
<i>The Guardian</i>	80	<i>Radio One</i>	64	<i>CG FM</i>	80	<i>Azam TV</i>	64	
<i>Jamhuri</i>	79	<i>Clouds FM</i>	65	<i>Highlands FM</i>	62	<i>Ayo TV</i>	40	
<i>Mwananchi</i>	84	<i>ZBC Radio</i>	69	<i>Arusha 1 FM</i>	84	<i>ZBC TV</i>	65	
<i>Nipashe</i>	65	<i>Zenji FM</i>			72			
<i>Zanzibar Leo</i>	80	<i>Micheweni FM</i>			55			
<i>Mwanahalisi</i>	80	<i>Safari FM</i>			63			
<i>Habari Leo</i>	78							
<i>Raia Mwema</i>	55							
<b>Total</b>	<b>757</b>		<b>342</b>		<b>540</b>		<b>288</b>	<b>80</b>

### 3.3 Sampuli ya kazi za kihabari

Utafiti huu ulitumia wiki ya kufikirika "artificial week" kama mbinu ya kupata sampuli ili kuhakikisha kwamba sampuli inayoteuliwa inawakilisha hali halisi ya jumla ya habari zilizokuwa zimeripotwa kwenye vyombo vya habari vya Tanzania. Siku kumi ndani ya wiki kumi zilichaguliwa. Kipindi cha wiki hizo kumi kilianza wiki ya mwisho ya Septemba, 2019 hadi wiki ya mwisho ya Novemba, 2019.

### Jedwali 3: Siku zilizochaguliwa kwenye sampuli

Siku	Tarehe	Siku	Tarehe
Jumanne wiki ya 1	24 Septemba	Jumapili wiki ya 6	3 Novemba
Jumatano wiki ya 2	2 Oktoba	Ijumaa wiki ya 7	8 Novemba
Alhamisi wiki ya 3	10 Oktoba	Jumatano wiki ya 8	13 Novemba
Ijumaa wiki ya 4	18 Oktoba	Alhamisi wiki ya 9	19 Novemba
Jumamosi wiki ya 5	26 Oktoba	Jumatatu wiki ya 10	25 Novemba

### 3.4 Uteuzi wa habari zilizoshughulikiwa

Kwenye magazeti, kazi nane za kihabari zilichaguliwa kila siku. Kazi hizi zilijumuisha habari zilizoandikwa ukurasa wa kwanza, habari kuu kwenye kila ukurasa, na makala. Habari za kimichezo hazikuchaguliwa. Kwenye Televisheni na redio, habari nne za mwanzo kwenye kila taarifa ya habari ya jioni zilichaguliwa pamoja na vipindi viwili au vitatu kwenye siku husika.

Kwenye mazingira ambapo ilikuwa vigumu kupata vipindi vyote kwenye siku husika, vipindi vilivyokosekana vilichaguliwa kutoka siku iliyofuatia ya wiki husika. Kwa vile vipindi vyenye vipengele mbalimbali, ni kipengele kimoja tu ndicho kilichoshughulikiwa.

Kwa *Jamii Forums*, utafiti huu ulitumia njia ya uteuzi maalumu. Katika mazingira hayo, kazi zilizokuwa zimewekwa kwenye mada mahsusi inayoendana na utafiti huu, mada mpya na mijadala vilichaguliwa kujumuishwa kwenye utafiti na michango iliyokuwa imetolewa kwa kila kazi ndani ya siku tatu za mwanzo baada ya uzinduzi wake zilichambuliwa. Kwa ujumla kazi 2,400 hatimaye zilipitiwa (taarifa 80 zilizokuwa zimewekwa na michango 30 iliyotolewa kwa kila taarifa).

### 3.5 Uteuzi na mafunzo kwa waandishi wafasiri (*transcribers*), wasimbaji (*coders*) na wachambuzi wa data

Kama ilivyokuwa mwaka 2018, kazi ya ufasiri (*transcription*) na usimbaji (*coding*) ilifanywa na makundi mbalimbali ya wasaidizi. Wasaidizi waliochaguliwa walipatiwa mafunzo kwa nyakati tofauti kwenye Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalipelekea kuingia mikataba na wafasiri kumi (10) na wasimbaji kumi na mmoja (11). Kando ya hao, kundi jingine la wasaidizi watatu lilifundishwa kwenye maeneo ya utakasaji data (*data cleaning*) na uchambuzi wa data.

### 3.6 Kurekodi kazi za kwenye redio na televisheni

Kabla ya kurekodi kazi za redio na televisheni, watafiti walipitia ratiba za vipindi vya redio na televisheni ili kuchagua vipindi vya kurekodi. Watu wa kurekodi vipindi vya redio za mikoani walitoka kwenye vyombo husika vya habari huku kazi ya

kurekodi kwenye redio na televisheni nyinginezo ilifanywa na mtu aliyetoka nje ya vyombo husika vya habari.

### 3.7 Udhibiti wa ubora wa kazi zilizorekodiwa na kufanyiwa usimbaji

Kazi ya kudhibiti ubora ilihusisha mchakato makini wa kuhakikisha kazi zote zilizorekodiwa zilikuwa kamilifu na zimepewa msimbo. Kazi zote za kihabari za kwenye magazeti na zile zilizoandikwa kutokana na kazi za kwenye redio na televisheni zilihifadhiwa kama rejea pindi pakihitajika kufafanua jambo lolote kuhusiana na usimbaji.

### 3.8 Uchunguzi na uchambuzi wa data

Baada ya kusimbwa data zilipitiwa upya ili kubaini usahihi wake na usawa na kisha kuwekwa kwenye faili jumuishi la SPSS. Uchambuzi ulitumia zana za kawaida za takwimu – idadi ya matukio (*frequency*) na upangilifu kimajedwali (*cross-tabulation*) ya kazi asilia na data iliyosimbwa (*re-coded*) upya kuhusu vigezo vya ubora.

## 4.0 MATOKEO

Picha ya jumla hapa chini inaonesha ubora kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018.

- Sampuli ya magazeti imeshuka katika ubora wake karibu katika vigezo vyote vya ubora ilihali kwa redio na televishe ni vimeboreshwa angalau katika baadhi ya vipengele vya vipindi vyao.
- Kushuka kwa kasi katika ubora kuna onekana katika uripoti kamilifu, kwani mawanda ya mitazamo (kuripoti kwa Sampuli ya magazeti imeshuka katika ubora wake karibu katika vigezo vyote vya ubora ilihali kwa redio na televishe ni vimeboreshwa katika baadhi ya vipengele (angalau kwenye vipindi vyao).
- Kushuka kwa kasi katika ubora kunaonekana katika uripoti kamilifu, kwani mawanda ya mitazamo (kuripoti kwa mtazamo mahsusi na wa kina) yameathirika zaidi ikilinganishwa na mwaka 2018 katika aina zote za vyombo vya habari.
- Sawa na hilo, idadi ya kazi za kihabari zenye maoni na mitazamo huru imeporomoka mno hata ikilinganishwa na kiwango cha chini kilichobainika mwaka 2018.
- Vyanzo vingi vya habari vimeathirika sana isipokuwa kwa vipindi vya redio.
- Maboresho makubwa yanaonekana katika kubainisha viini vya matukio na changamoto kwa sababu vipindi vya redio na televisheni viliripoti zaidi kwenye eneo hilo kwa mwaka 2019 kuliko ilivyokuwa mwaka uliotangulia.
- Eneo lingine lililoboreshwa miongoni mwa tanzu zote za vyombo vya habari ni uripoti wa takwimu. Mwaka 2019, vyombo vya habari viliboresha kuzielezea takwimu husika kwenye muktadha fulani na kuzifanya siyo tu zipatikane bali pia zieleweke na hadhira. Kuhusiana na uripoti habari za matukio, hali imeimarika ingawa ni kwa kiasi kidogo tu ikilinganishwa na mwaka 2018.

### Jedwali 4: Matokeo ya mwaka 2019 dhidi ya ubora wa mwaka 2018

Mgawanyiko	Vyombo vyote vya habari		Redio		TV		Magazeti
			Habari	Vipindi	Habari	Vipindi	
Mazingira ya upatikanaji habari	▲ +2%		▲ +2%	▲ +9%	▲	—	▼ -6%
Vyanzo vya habari	▼ -5%		▼ -11%	▲ +3%	—	▼ -11%	▼ -9%
Vyanzo vya habari vyenye jinsi ya kike	▼ -2%		▼ -6%	▼ -6%	—	▲ +12%	▼ -2%
Mzizi wa habari	—		—	▲ +9%	▼	▲ +13%	▼ -10%
Mitazamo ndani ya habari	▼ -11%		▼	▼ -9%	▼ -3%	▼ -13%	▼ -18%
Maoni ndani ya habari	▼ -10%		▼ -3%	▲ +2%	—	▼ -21%	▼ -29%
Maoni kinzani ndani ya habari	▼		—	▼	—	—	▼
Matumizi ya takwimu na muktadha wake	▲ +17%		▲ +30%	▲ +30%	—	—	▲ +6%
Haki ya kujibu tuhuma	▼ -11%		▼ -10%	▼ -10%	▼ -6%	▼ -6%	▼ -16%
Muundo wa uandishi wa habari	▼		▲ +4%	▲ +4%	▼ -4%	▼ -4%	▼ -10%


## 4.1 Muktadha wa uripoti wa habari

Kiashiria hiki kinaangalia kama uripoti wa habari ni zao la habari za matukio au ikiwa ni jitihada binafsi za waandishi wa habari.

## Vyombo vyote vya habari

Kwa wastani, uripoti unaozingatia matukio bado umebaki zaidi ya nusu ya habari zote zilizo chambiwa (asilimia 58), lakini umeshuka kidogo kwa pointi asilimia mbili. Redio za kitaifa zimejitahidi kupanua uripoti unaozingatia jitihada binafsi (habari zisizo za matukio), lakini jitihada za magazeti zilishuka. Televisheni na redio za kimikoa zilishuhudia ongezeko kidogo tu.

## 2019: Mazingira ya upatikanaji habari




### Taarifa za habari za redioni

Mwaka 2019, radio zilikuwa na habari nyingi kwenye taarifa za habari ambazo wamezitaifuta wenyewe kutoka asilimia 17 mwaka 2018 hadi asilimia 28 mwaka 2019. Redio za mikoani ambazo tayari zilikuwa na uripoti mwingi wa agenda zao, kwa mwaka 2019 ziliongeza kiwango hicho. Kwa *Pangani FM*, *Dodoma FM*, na *CG FM* idadi iliongezeka bayana kabisa (vituo vyote vitatu vina zaidi ya asilimia 40 ya habari walizozitaifuta wenyewe, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 15). Redio zingine za mikoani zilifikia

kiwango cha karibu asilimia 38 (*Highlands FM*, *Arusha 1 FM*, na *Zenj FM*). Kwa upande mwingine, *TBC Taifa* na *Clouds FM* zingali zikitungia zaidi habari za matukio kwenye taarifa zao za habari (asilimia 87, na asilimia 89 mtawalia), wakati redio nyingine za kitaifa zikishuhudiwa kushuka mno, kama ilivyoonekana kwa *Radio Free Africa* (77%), *Radio One* (72%) na *ZBC Radio* (67%). Ni redio chache tu za mikoani (*Micheweni FM*, *Safari FM*) zilizoonyesha kutegemea habari za matukio kwa wingi katika taarifa zao za habari kwa kiwango cha asilimia 80 na 85 mtawalia.

## 2019: Upatikanaji wa habari kwenye taarifa za habari za radio




### Vipindi vya radio

Vipindi vya radio hutayarishwa kwa kutegemea zaidi jitihada za wanahabari (na sio matukio) kwa asilimia 73. Radio za *Pangani FM* na *Micheweni FM* zilifikia asilimia 100 katika kipengele hiki zikifuatiwa na *ZBC Radio* (asilimia 87), *Dodoma FM* (asilimia 83), *CG FM* (asilimia 81) na *Highlands FM* (asilimia 75). Zilizokuwa chini ya wastani ni *TBC Taifa* (asilimia 72) na *Radio Free Africa* (asilimia 59), lakini vyote viwili viliongezeka vya kutosha ikilinganishwa na mwaka 2018. Radio One ilibaki kwenye kiwango kilekile (asilimia 72) *Clouds FM* vilevile (asilimia 50), lakini ni kwa viwango vya chini. *Arusha 1 FM* ilipata alama za chini zaidi miongoni mwa radio za mikoani.

Ikilinganishwa na mwaka 2018, vipindi vya radio vimeboreshwa kwani nafasi yao ya uripoti vipindi vitokavyo na habari za matukio iko chini kwa asilimia 27 kwa mwaka 2019, ikilinganishwa na asilimia 33 kwa mwaka 2018.

## 2019: Mazingira ya upatikanaji habari kwenye vipindi vya radio






## Televisheni

Uripoti wa habari kwenye TV mara zote umekuwa ukiongozwa na habari za matukio huku vipindi vyake vikiongozwa na jitihada binafsi za vyombo husika. Kwa mwaka 2019, TBC 1, ITV na Azam TV viliongeza kidogo hisa zao za uripoti wa habari kwenye taarifa zao za habari kwa kutafuta

habari zao wenyewe kwa asilimia 13, 17 na 20, huku Ayo TV na ZBC TV vikitegemea mno kwenye suala hilo (kwa asilimia 6 na 3). Kwenye vipindi hali iko tofauti. Vituo vyote vya televisheni hutegemea zaidi jitihada zao binafsi kwa zaidi ya asilimia 90%, huku ITV ikiongoza kwa asilimia 100.

## 2019: Habari za matukio na zisizo za matukio kwenye TV




## Magazeti

Hapa kuna utofauti bayana kabisa kati ya magazeti yanayotoka kila wiki na yanayotoka kila siku. Magazeti ya kila wiki mara nyingi hufuata agenda zao (*Jamhuri* asilimia 82, *Raia Mwema* asilimia 83) huku yale ya kila siku hufuata zaidi habari za matukio. Kwa wastani, uripoti wa kwenye magazeti unaofuata jitihada zao wenyewe kwa mwaka 2019 ulikuwa wa asilimia 33 tu, zikishuka kwa asilimia 6 kutoka asilimia 39 za mwaka 2018. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa hapa. *The Guardian* hufuata zaidi

habari za matukio (asilimia 85, ongezeko la asilimia 4 kutoka mwaka 2018), na *Daily News* ilikuwa asilimia 83 (ongezeko la asilimia 19 kutoka mwaka 2018). *Zanzibar Leo* (asilimia 80 dhidi ya 70) na *The Citizen* (asilimia 64 dhidi ya 53) zimeongeza uripoti wao wa habari za matukio. Vyombo vya habari viwili tu ndivyo vilipunguza utegemezi wa habari za matukio kwa mwaka 2019 ambavyo ni *Mwananchi* (54% zikipungua kwa asilimia 3) na *Jamhuri* (18% zikipungua kwa 19%).

## Magazeti: Habari za matukio na zisizo za matukio




### 4.2 Hali ya uripoti kwa mada

Tafti hii huchunguza habari husika inahusu mada gani kutoka miongoni mwa mada 38. Mada zimefupishwa kwenye masuala saba (7):

- o Ajali/ uhalifu: Ajali, uhalifu, kesi za mahakamani, majanga.
- o Masuala ya maendeleo: Afya, Elimu, Kilimo, Uvuvi na Usalama wa Chakula. Mazingira na uchafuzi wa mazingira, mabadiliko ya tabia za nchi, maji na usafi.
- o Masuala ya kisiasa: Sera, siasa, uchaguzi, usalama wa taifa.
- o Masuala ya kiuchumi: Miundombinu, mafuta, gesi na uchimbaji madini, mawasiliano, Benki na Fedha, uzalishaji viwandani, ajira, takwimu za biashara, utalii, n.k.
- o Utamaduni/vyombo vya habari: Vyombo vya habari, utamaduni, dini.
- o Masuala yenye mpishano wa mawazo: Migogoro, matatizo ya kijamii, rushwa, wakimbizi, haki za binadamu, migogoro ya kijinsia, utawala bora na uwajibikaji.
- o Utafti: Utafti









Kwa mwaka 2019, uripoti kwenye masuala ya kisiasa uliongezeka hadi kufikia asilimia 16.8 ikilinganishwa na asilimia 10.9 mwaka 2018. Uripoti kwenye masuala yaliyohusu mpishano wa fikra (*contentious issues*) uliongezeka kwa pointi 2%. Uripoti kwenye masuala ya kiuchumi ulishuka kwa pointi asilimia 8. Masuala ya kimaendeleo yalibaki vilevile, kama ilivyokuwa kwenye uripoti wa uhalifu na ajali.

## Mada zilizoripotiwa na vyombo vya habari



### Mada zilizoripotiwa

Kwa mwaka 2019, uripoti kwenye masuala ya kisiasa uliongezeka hadi kufikia asilimia 16.8 ikilinganishwa na asilimia 10.9 mwaka 2018. Uripoti kwenye masuala yaliyohusu mpishano wa fikra (*contentious issues*) uliongezeka kwa pointi 2%. Uripoti kwenye masuala ya kiuchumi ulishuka kwa pointi asilimia 8. Masuala ya kimaendeleo yalibaki vilevile, kama ilivyokuwa kwenye uripoti wa uhalifu na ajali



### 4.3 Vyanzo vingi vya habari

Kigezo hiki kilichunguza ni vyanzo vingapi vya habari vimetajwa kwenye kazi husika ya kihabari. Waandishi au watangazaji wenyewe hawahesabiki kama vyanzo vya habari. Vile vile wanaopiga simu kwenye vipindi vya redio au televisheni hawahesabiki kama vyanzo vya habari bali kama wachangiaji.


Kazi ya kihabari (magazeti, redio, televisheni, vyombo vya habari vya mtandaoni) inapaswa kuwa na angalau vyanzo viwili vya habari husika. Hata hivyo, kazi nyingi kati ya zilizofanyiwa utafiti hasa matangazo ya vipindi na maoni zilikuwa na ama chanzo kimoja cha habari au hakikuwepo kabisa.

### Vyombo vyote vya habari

Kwa mwaka 2019, asilimia 40 ya sampuli yote iliyochunguzwa ilikuwa na chanzo kimoja cha habari. Kigezo cha chini kabisa cha kuwa na vyanzo viwili vya habari au zaidi kilitimizwa kwa asilimia 60 tu ya sampuli zilizochunguzwa. Magazeti yanaongoza katika kipengele hiki (asilimia 68), yakifuatiwa na redio za kitaifa (asilimia 58), Televisheni (asilimia 56) na redio za mikoani (asilimia 55).

Tukifanya ulinganisho, tatizo la kutokuwa na vyanzo vingi vya habari linaonekana kuongezeka kwani vyombo vyote vya habari vilipata alama za chini kwenye kipengele hicho mwaka 2018. Vyombo vyote vya habari vimetumia vyanzo vichache vya habari ikilinganishwa na mwaka 2018, kwa wastani ni upungufu wa asilimia 4 katika kutumia “vyanzo viwili au zaidi”.

### Vyanzo vya habari




### Taarifa za habari za redio

Kwa taarifa za habari za redioni, matumizi ya vyanzo viwili au zaidi vya habari ilishuka kwa redio zote kutoka asilimia 58 hadi asilimia 49. Hata hivyo, habari za redioni zimeonesha utofauti wa aina mbalimbali miongoni mwa vituo vya redio katika utumiaji wa vyanzo vya habari. Wanaoongoza katika kipengele hiki ni *Micheweni FM* (asilimia 84) na *Radio Free Africa*

(asilimia 75). Kinyume chake, *Arusha 1 FM* (asilimia 21), *Safari FM* na *Highlands FM* vyote vilipata asilimia 34 vikipata alama za chini kama ilivyobainishwa. Vituo vingine vya redio viko katikati (kutoka asilimia 40 hadi asilimia 55). Ikilinganishwa na mwaka 2018, *Radio One* ilipoteza zaidi (kwa asilimia pungufu ya 30). *Clouds FM* ilishuka kwa asilimia 14, huku *Pangani FM* na *Dodoma FM* zikibakia katika hali ile ile.


## 2019 Habari za redio: Vyanzo viwili au zaidi



### Vipindi vya redio

Kwa taarifa za habari za redioni, matumizi ya vyanzo viwili au zaidi vya habari ilishuka kwa redio zote kutoka asilimia 58 hadi asilimia 49. Hata hivyo, habari za redioni zimeonesha utofauti wa aina mbalimbali miongoni mwa vituo vya redio katika utumiaji wa vyanzo vya habari. Wanaoongoza katika kipengele hiki ni *Micheweni FM* (asilimia 84) na *Radio Free Africa* (asilimia 75). Kinyume chake, *Arusha 1 FM* (asilimia 21), *Safari FM* na *Highlands FM* vyote vilipata asilimia 34 vikipata alama za chini kama ilivyobainishwa. Vituo vingine vya redio viko katikati (kutoka asilimia 40 hadi asilimia 55). Ikilinganishwa na mwaka 2018, *Radio One* ilipoteza zaidi (kwa asilimia pungufu ya 30). *Clouds FM* ilishuka kwa asilimia 14, huku *Pangani FM* na *Dodoma FM* zikibakia katika hali ile ile.

## 2019 Vipindi vya redio: Vyanzo 2 au zaidi



## Televisheni


Kwa upande wa televisheni, kuna utofauti mkubwa kati ya habari na vipindi katika kutumia vyanzo vya habari zaidi ya kimoja na utofauti miongoni mwa vituo vya televisheni. Ikilinganishwa na radio, televisheni zilifanya vizuri katika kutumia chanzo zaidi ya kimoja kwenye habari (asilimia 57 ikiwa na vyanzo viwili na zaidi) kuliko kwenye vipindi (asilimia 55).

Kwa habari, *ITV* inaongoza kutumia vyanzo vingi kwenye habari kwa asilimia 91, ikifuatiwa na *TBC1* (asilimia 62), *Azam TV* (asilimia 61), na *ZBC TV* (asilimia 53). *Ayo TV* inafuatia kwa mbali ikiwa na asilimia 20 tu ya habari zake zikiwa na chanzo zaidi ya kimoja (hata hivyo zaidi ya ilivyokuwa mwaka

2018). Kwenye vipindi, *ZBC TV* inaongoza ikiwa na asilimia 63, ikifuatiwa na *Azam TV* (asilimia 57), *ITV* (asilimia 51) na *TBC 1* (asilimia 40).

Kwa upande wa mabadiliko, kwa wastani vituo vya televisheni vilitumia vyanzo vichache zaidi vya habari mwaka 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018 (kwa zaidi ya asilimia 11 ya takwimu za 2018). Ni *ITV* pekee iliyopandisha alama zake katika kipengele cha kutumia vyanzo viwili au zaidi vya habari kwa pointi asilimia 8 kwenye habari zake. Vituo vingine vya televisheni vilipata alama za chini katika kipengele hiki. Kwenye vipindi, vituo vyote vya televisheni vilipata alama za chini katika matumizi ya chanzo zaidi ya kimoja. *TBC 1* ikifanya vibaya zaidi, (pungufu kwa 20%). *ITV* na *Azam TV* vyote vikipata alama zaidi ya 10%.

## 2019 TV: Vyanzo 2 na zaidi




## Magazeti

Kwa mwaka 2019 kulikuwa na idadi ya kutosha - 24 katika ujumla wake - ya habari zisizokuwa na chanzo chochote (ongezeko kutoka 13 mwaka 2018). Nyingi ya habari hizi zilikuwa kwenye gazeti la *Jamhuri* (7) na *Raia Mwema* (15), yote ni magazeti yanayotoka kila wiki. Mengine ni *The Citizen* (1) na *Nipashe* (1).

Kwa wastani habari zilizokuwa na vyanzo vingi vya habari kwenye magazeti zilikuwa asilimia 68 ambazo ni pungufu kwa asilimia 9 ukilinganisha na mwaka 2018 (asilimia 77). Hata hivyo, kuporomoka huku hakuonekani kwenye magazeti yote. *Mwananchi* lilishika nafasi nzuri likiwa na asilimia 85 (pungufu kwa asilimia 1) likifuatiwa na *The Guardian* (asilimia 77), *The Citizen* (asilimia 75), *Daily News* (asilimia 73) na *Nipashe* (asilimia 70). *Jamhuri* (asilimia 59), *Mwanahalisi* (asilimia 55), *Habari Leo* (asilimia 63) na *Raia Mwema* (asilimia 35) yalifanya vibaya katika kipengele hiki. *Zanzibar Leo* pia lilifanya vibaya kwa asilimia 10.

## Magazeti 2019: Vyanzo viwili au zaidi



### 4.4 Wanawake kama vyanzo vya habari


IKwenye kipengele hiki, utafiti unachunguza ni wanawake wangapi wametajwa (na wanaonekana bayana) kama vyanzo vya habari kwenye makala, habari au kipindi.

#### Vyombo vyote vya habari

Wanawake hawakuonekana kuwa sehemu ya vyanzo vya habari kwa mwaka 2019. Kwa wastani, asilimia 66 ya habari zote zilizochunguzwa hazikuwajumuisha wanawake kama vyanzo vya habari. Jumla ya asilimia 22 ya habari zilikuwa na mwanamke mmoja kama chanzo cha habari na asilimia 12 zilikuwa na wanawake wawili au zaidi. Magazeti yanaonekana kufanya vibaya zaidi katika eneo hili. Redio za mikoani zilifanya vizuri zikipata asilimia 18 ya habari zake zikiwa na wanawake wawili au zaidi kama vyanzo vya habari.

Kwa mwaka 2018, matokeo ya ujumla yalikuwa sawa, imeshuka kidogo tu mwaka 2019 huku ikiwa ni pungufu kwa pointi asilimia 1 au 2.

### Vyanzo vya habari vya jinsia ya kike



## Habari za redioni

Kwenye taarifa za habari za redioni, idadi ya habari ambazo hazikuwa na mwanamke yeyote kama chanzo cha habari zilikuwa asilimia 72. Jumla ya asilimia 20 zilikuwa na mwanamke mmoja, na asilimia 8 ilikuwa na wawili. Redio za mikoani kama *Micheweni FM* na *Pangani FM* zilifanya vizuri katika eneo hili kwa asilimia 51 na asilimia 42 ya habari zake zikiwa na angalau mwanamke mmoja kama chanzo cha habari. *Radio One* (asilimia 12) na *Safari FM* (asilimia 14) ndivyo vyombo vilivyokuwa mkiani.

## Vipindi vya redio

Uwakilishi wa sauti za wanawake uko vizuri kidogo kwenye eneo hili. Hata hivyo bado asilimia 52 ya vipindi haikuwa na wanawake kama vyanzo vya habari, asilimia 22 ilikuwa na mwanamke mmoja. Ni asilimia 26 tu iliyokuwa na wanawake wawili kama chanzo.

*Pangani FM* ndiyo iliyofanya vizuri zaidi katika eneo hili kwa asilimia 88 ya vipindi vyake kuwa na wanawake wawili au zaidi kama chanzo cha habari ikifuatiwa na *Micheweni FM* yenye asilimia 58, na *Dodoma FM* yenye asilimia 39. Wa chini kabisa kwenye kipengele hiki ni *Clouds FM* (asilimia 11), *Radio One* (asilimia 13) na *ZBC Radio* (asilimia 14). Baadhi ya redio zinahitaji kuongeza juhudi kwani zina asilimia kubwa mno ya ripoti zikiwa hazina mwanamke aliyetumika kama chanzo cha habari. Hizi ni *Highlands FM* (asilimia 76), *ZBC Radio* (asilimia 64), *Radio Free Africa* (asilimia 61) na *Radio One* (asilimia 59).

Ikilinganishwa na mwaka 2018, matumizi ya wanawake kama vyanzo vya habari yameshuka kwa karibu asilimia 6 ikiangaliwa pamoja kwenye habari na vipindi. Asilimia ya habari zisizokuwa na mwanamke kama chanzo cha habari imeongezeka japokuwa asilimia za zile zenye mwanawake 1 au 2 na zaidi kama vyanzo vya habari ilishuka.

## Jedwali 5: Wanawake kama vyanzo vya habari kwenye redio

Mwaka	Hakuna chanzo	Chanzo 1	Vyanzo 2 na zaidi
2018	57%	27%	17%
2019	64%	21%	16%

## Televisheni

Kwenye taarifa za habari za Televisheni, kulikuwa na wanawake wachache waliotumika kama vyanzo vya habari kuliko katika vipindi. Katika taarifa za habari, *ITV* ilifanya vizuri ikiwa na asilimia 47 tu ya habari zilizochunguzwa ambazo hazina wanawake kama vyanzo vya habari. *TBC 1*, *AZAM TV* na *Ayo TV* zina zaidi ya asilimia 70 ya habari zisizo na wanawake kama vyanzo vya habari. Wastani wa asilimia 68, kama ilivyokuwa mwaka 2018.

Kwa upande wa vipindi, hali haikuwa tofauti na taarifa za habari na vipindi vya redioni. Kwenye Televisheni, asilimia 55 ya vipindi havikuwa na wanawake kama vyanzo vya habari, asilimia 31 zilikuwa na mmoja, na asilimia 15 zilikuwa na wanawake wawili au zaidi waliotumika kama vyanzo vya habari.

Televisheni iliyofanya vizuri zaidi katika eneo hili ni *TBC 1*, kwani ilikuwa na asilimia kubwa ya "wanawake 2 au zaidi kama vyanzo vya habari" (asilimia 27), ikifuatiwa na *Azam TV* (asilimia 18). Televisheni ya mwisho ni *ZBC TV* ambayo asilimia 61 ya taarifa zake hazikuwa na wanawake kama vyanzo vya habari na asilimia 9 tu ya taarifa zake ndizo zilikuwa na wanawake wawili kama vyanzo vya habari.

Ikilinganishwa na mwaka 2018, utumiaji wa wanawake kama vyanzo vya habari katika mwaka 2019 uliboreshwa katika vipindi vya Televisheni. Kwa wastani, vipindi vya televisheni kwa mwaka 2019 vilikuwa na asilimia 10 pungufu ya vipindi visivyokuwa na mwanamke hata mmoja kama chanzo cha habari na asilimia 12 vikiwa na mwanamke mmoja kama chanzo cha habari.



## Magazeti

Katika magazeti, asilimia 70 ya habari hazikuwa na mwanamke kama chanzo cha habari. Jumla ya asilimia 21 zilikuwa na mwanamke mmoja kama chanzo cha habari na asilimia 9 zilikuwa na wawili au zaidi. Magazeti yaliyofanya vizuri zaidi ni The Guardian (lililokuwa na asilimia 53 tu ya habari zisizo kuwa na wanawake kama vyanzo vya habari), Daily News na Zanzibar Leo (yote mawili yalikuwa na asilimia 60 ya habari ambazo hazikuwa na wanawake kama vyanzo vya habari). The Guardian (asilimia 14), Daily News (asilimia 13) na Habari Leo (asilimia 13) yalifanya vizuri kwa kuwa na wanawake 2 au zaidi kama vyanzo vya habari. Magazeti ya *Raia Mwema*, *Jamhuri*, *The Citizen* na *Mwanahalisi* yalifanya vibaya sana kwani yalikuwa na kati ya asilimia 2 na 5 ya habari zilizokuwa na wanawake wawili na zaidi kama vyanzo vya habari.

Ikilinganishwa na mwaka 2018, ubora wa magazeti katika hili ulishuka mwaka 2019 ingawa ni kwa tofauti ndogo ya upungufu wa asilimia 2 ya wanawake kama vyanzo vya habari.

### 4.5 Idadi ya mitazamo

Wasimbaji (*coders*) walitathimini ni 'mitazamo' (perspectives) ipi inaelezewa katika taarifa fulani ya habari. Hii ni pamoja na mitazamo inayogusa masuala ya kawaida ya wananchi, kisera, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiusalama. Kwa namna yoyote iwayo, mtazamo utaonekana kuwepo ikiwa tu habari inafafanua suala husika katika mtazamo huo. Kutaja tu baadhi ya maneno kutoka katika maeneo ya kiuchumi, au kisiasa haitoshi kuchukuliwa kuwa ni mtazamo. Hii ni ishara kuwa habari fulani angalau zinaripoti suala fulani kwa kina.

Kuripoti kwa mtazamo fulani mahsusi humaanisha kwamba baadhi ya masuala (Ya kiuchumi, kisiasa, ya kawaida kuhusu jamii, ya kisayansi na mengineyo) kwenye habari husika yamechukuliwa kwa uzito hivyo kuripotiwa kwa kina. Ni kinyume cha kuripoti habari juu juu – huku ukitoa taarifa za msingi.

### Vyombo vyote vya habari


Katika sampuli yote, kulikuwa na makala nyingi zisizokuwa na mtazamo wowote. Hii ina maana kwamba utoaji wa habari aghalabu huwa ni wa juu-juu na hasahasa hulenga zaidi katika tukio au suala fulani mahsusi. Utoaji wa habari hauchunguzi kona fulani mahsusi kama vile athari za kiuchumi au kisiasa za jambo au tukio fulani. Kwa maneno mengine, utoaji wa habari haukuwa wa kina.

Kwa mwaka 2019, uripoti habari kwa kuzingatia mitazamo ulikuwa duni. Kwa wastani, asilimia 40 ya habari zilichambuliwa hazikuonesha upana na kina kuhusiana na suala la mtazamo. Kwa upande wa aina za vyombo vya habari, Televisheni zilikuwa na habari nyingi zaidi (asilimia 48) zisizo na

mtazamo wowote. Tofauti pekee ilikuwa ni kwa JamiiForums ambayo ilikuwa na asilimia 8 tu ya habari zake zisizokuwa na mtazamo. Sehemu kubwa (asilimia 40) ya taarifa zake zilikuwa na mitazamo miwili au zaidi.

Kipengele hiki cha ubora wa utoaji wa habari kwa kuzingatia mtazamo/mitazamo fulani mahsusi kilishuka mwaka 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018. Kwa wastani, mwaka 2018 kulikuwa na asilimia 23 tu ya habari zisizokuwa na mtazamo wowote, na asilimia 64 zilikuwa na angalau mtazamo mmoja, ikilinganishwa na asilimia 53 tu katika mwaka 2019. Aidha, kutokuwepo kwa mitazamo ni moja ya changamoto kubwa zinazovikabili vyombo vya habari nchini Tanzania.

### 2019: Idadi ya mitazamo kwenye habari na vipindi




## Taarifa za habari za redioni

Kwenye taarifa za habari za redioni, asilimia ya ripoti zisizo na mtazamo mahsusi zilikuwa asilimia 49. Radio One ina idadi kubwa ya taarifa za habari zisizo na mtazamo zinazofikia asilimia 72. Redio zilizofanya "vizuri zaidi" ni *CG FM* (asilimia 34) na *Clouds FM* (asilimia 30). Kwa wastani, asilimia 47 ya ripoti zilikuwa na mtazamo mmoja. Kwa mara nyingine *Clouds FM* (asilimia 67) na *CG FM* (asilimia 59) zilifanya vizuri zaidi katika kipengele hiki.

Umahiri katika eneo hii ulipungua hadi kufikia asilimia 47 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 58 mwaka 2018. Hali hii ilitokana na alama za *Radio Free Africa*, *Radio One*, *CG FM*, na *Arusha 1 FM* kuporomoka katika kipengele hiki. Alama za *Dodoma FM* na *Micheweni FM* ziliendelea kubaki pale pale, wakati *Clouds FM* ikipanda. *Pangani FM* yenyewe ilishuka kabisa.

## Idadi ya mitazamo kwenye taarifa za habari za redio



## Vipindi vya redio

Kwa upande wa vipindi vya redio, idadi ya habari "zisizo na mtazamo" zilifikia asilimia 29, ikilinganishwa na asilimia 20 za mwaka 2018. Redio iliyo-fanya vibaya zaidi katika eneo hili ni *ZBC Radio* (asilimia 43 hazina mitazamo), *Arusha 1 FM* (asilimia 40), *CG FM* (asilimia 34) na *TBC Taifa* (asilimia 33).

Kuripoti mtazamo mmoja ni hitaji la msingi kwa vyombo vyote vya habari, na ni asilimia 59 tu ya habari zilikuwa na mtazamo mmoja mwaka 2019. Nyingine zilizosalia, asilimia 12 zilikuwa na mitazamo miwili au zaidi. *Dodoma FM* ilikuwa na asilimia kubwa katika kuwa na mtazamo mmoja (asilimia 91), ikifuatiwa na *Pangani FM* (asilimia 71), *Micheweni FM* (asilimia 67), na *Radio Free Africa* (asilimia 68). Hata hivyo, baadhi ya vituo


vya redio vilifanya vizuri zaidi na wakati mwingine vilikuwa na mitazamo miwili. Vituo hivi ni *Micheweni FM*, *TBC Taifa* na *Safari FM* (vyote asilimia 21), vikifuatiwa na *Clouds FM* na *Pangani FM* (vyote viwili asilimia 18), *Radio One* (asilimia 16) na *Zenji FM* (asilimia 14).

Ufanisi katika hili ulikuwa mzuri zaidi mwaka 2018 ukiwa na wastani wa asilimia 67 wa habari zenye mtazamo mmoja, na asilimia 14 zenye mitazamo miwili au zaidi.

Ingawa mwonekano wa jumla ulionyesha kwamba ubora ulikuwa wa kiwango cha chini, baadhi ya vituo vya redio viliendelea kubaki katika viwango vilevile au kuboreshwa mwaka 2019. Maboresho makubwa yalionekana kufanywa na *Clouds FM* (kutoka katika kiwango cha chini kabisa mwaka 2018) na *Radio One*. Redio

ambazo matokeo yao hayakubadilika ni *Micheweni FM*, *Pangani FM*, *Dodoma FM* na *Highlands FM*. Redio nyingine (ZBC Radio, Zenj FM, Radio Free Africa, na Arusha 1 FM) zilishuka viwango katika kipengele cha uripoti unaozingatia mtazamo fulani.

## Idadi ya mitizamo kwenye vipindi vya redio



## Televisheni

● Mitizamo 2 au zaidi ● Mtazamo 1 ● Hakuna mtazamo


Kwa upande wa habari za Televisheni, asilimia 64 ya habari zilichambuliwa hazikuwa na mtazamo wowote, na asilimia 35 zikiwa ni habari zenye mtazamo mmoja tu. *ITV* ilionyesha utendaji mzuri ambapo ilikuwa na asilimia 47 ya habari zenye mtazamo mmoja, ikifuatiwa na *Azam TV* kwa asilimia 28, na *TBC1* ikiwa na asilimia 27.

Kwa upande wa vipindi vya Televisheni, kulikuwa na asilimia 22 tu za habari zisizokuwa na mtazamo, asilimia 70 zenye mtazamo mmoja, na asilimia 8 zikiwa na


mitazamo miwili au zaidi. *ZBC TV* na *TBC1* zilifanya vizuri zaidi kuliko *ITV* na *Azam TV* katika eneo hili, zikiwa na asilimia 18 tu ya habari zake zisizo na mtazamo. *TBC1* pia ilitoa taarifa nyingi zaidi zenye mitazamo miwili (asilimia 14) ikilinganishwa na *ZBC TV* (asilimia 9).

Mwaka 2018, asilimia 21 ya vipindi vilikuwa na mitazamo miwili, ikilinganishwa na asilimia 8 tu kwa mwaka 2019. *ITV* na *Azam TV* zilifanya vizuri zaidi katika kujumuisha mitazamo miwili kwenye taarifa za habari na vipindi kuliko vyombo vingine vya habari.

## 2019: Idadi ya mitizamo kwenye habari za TV



## Wastani



## Magazeti


Mwaka 2019, magazeti mengi yalikuwa na habari nyingi (wastani wa asilimia 40) zilizokuwa na uripoti wa juu-juu (= kutokuwa na mtazamo). Magazeti yaliyofanya vibaya zaidi katika hili yalikuwa Habari Leo na *Daily News* (yote mawili asilimia 51) na *Zanzibar Leo* (asilimia 43). *The Guardian* na *Nipashe* (yote mawili asilimia 41), *Mwananchi* (asilimia 39) na *Jamhuri* (asilimia 38). Gazeti lililofanya vizuri katika eneo hili ni *The Citizen* ambalo lilikuwa na asilimia 26.

Kazi za kihabari zilizokuwa na mtazamo mmoja zilikuwa na wastani wa asilimia 55, na zile zenye mitazamo miwili ni asilimia 5 tu. *The Citizen* liliongoza katika kuwa na habari zenye mtazamo mmoja

(asilimia 69), likifuatiwa na *Mwanahalisi* (asilimia 62), *Raia Mwema* (asilimia 60), *Mwananchi* na *Zanzibar Leo* (yote mawili asilimia 56). Magazeti yenye asilimia za chini yalikuwa *Daily News* (asilimia 41) na *Habari Leo* (asilimia 46). Habari nzuri zenye mitazamo miwili au zaidi ni chache sana, ambapo nzuri zaidi zikiwa ni za *Jamhuri* (asilimia 11), likifuatiwa na *Daily News* (asilimia 8) na *Nipashe* (asilimia 7).

Ikilinganishwa na mwaka 2018, ufanisi katika utoaji wa mitazamo katika habari ulishuka kwa kasi sana mwaka 2019. Kulikuwa na upungufu wa asilimia 6 kwa habari zenye mtazamo mmoja na upungufu wa 18% kwa habari zenye mitazamo miwili au zaidi. Magazeti yote yalikuwa na habari chache sana zenye mitazamo miwili. Habari nyingi zilikuwa na mtazamo mmoja tu.

## 2019: Idadi ya mitazamo kwenye habari za magazeti



### 4.6 Maoni

Kwa muktadha wa utafiti huu, maoni ni mawazo yanayotolewa na vyanzo vya habari au wahusika katika habari. Inahusisha matamko yaliyo wazi na yenye kuegemea upande fulani katika mwelekeo hasi au chanya. Huchunguzwa kazi ya kihabari ilikuwa na maoni mangapi. Kama ilivyokuwa kwenye ujumuishwaji wa mitazamo (perspectives) katika habari, vyombo vya habari havikufanya vizuri sana katika suala la kujumuisha maoni kwenye kazi zao. Maoni ni maelezo ya vyanzo vya habari yaliyo wazi na yenye kuegemea upande fulani kwa hiyo hutoa kauli yenye mwelekeo fulani kuhusu suala fulani. Maoni mbalimbali huchangia katika kuwafungua macho watumiaji wa vyombo vya habari na kuimarisha umma.

## Vyombo vyote vya habari

Kwa mwaka 2019, uwasilishaji wa maoni ulikuwa wa chini sana ambapo asilimia 60 ya habari zilizochembuliwa hazikuwa na maoni kabisa. Asilimia ishirini na tano (25) zilikuwa na maoni moja tu, na asilimia 15 zilikuwa na maoni mawili au zaidi. Huu ni upungufu wa karibu pointi asilimia 10 kutoka zile za 2018 ambapo asilimia 26 ya habari zilizochunguzwa zilikuwa na maoni 2 au Zaidi na asilimia 50 hazikuwa na maoni yoyote. Mwaka 2018 hitimisho lilikuwa kwamba utendaji wa vyombo vya habari katika eneo hili unahitaji kuboreshwa. Mwaka 2019 hali ilikuwa mbaya Zaidi. Jedwali hapa chini linaonyesha hali ilivyokuwa kuhusiana na maoni au kauli za maamuzi (judgemental statements) karibu katika kila chombo cha habari.

### Jedwali: Idadi ya habari zisizokuwa na maoni ndani yake kwenye magazeti

Magazeti	2018	2019	Mabadiliko
The Citizen	39%	59%	+20% ▼
The Guardian	55%	70%	+15% ▼
Mwananchi	29%	59%	+ 31% ▼
Daily News	40%	81%	+ 40% ▼
Nipashe	43%	77%	+34% ▼
Jamhuri	31%	54%	+22% ▼
Zanzibar Leo	41%	63%	+ 22% ▼
Mwanahalisi	-	29%	- ▲
Habari Leo	-	83%	- ▲
Raia Mwema	-	63%	- ▲

### TV: Idadi ya habari na vipindi visivyokuwa na maoni ndani yake


TV	2018	2019	Mabadiliko
TBC 1	54%	66%	+ 13% ▼
ITV	51%	75%	+24% ▼
Azam TV	52%	75%	+ 23% ▼
Ayo TV	50%	92%	+ 42% ▼
ZBC TV	-	36%	- ▲

### Idadi ya habari na vipindi visivyokuwa na maoni ndani yake kwenye redio

Kituo cha redio	2018	2019	Mabadiliko
TBC Taifa	76%	54%	-22% ▲
Radio Free Africa	56%	69%	+14% ▼
Radio One	67%	47%	-30% ▲
Clouds FM	75%	49%	- 25% ▲
Pangani FM	39%	53%	+14% ▼
Dodoma FM	63%	55%	+ 8% ▼
CG FM	37%	71%	+34% ▼
Highlands FM	52%	43%	- 9% ▲
Arusha 1 FM	61%	54%	+ 6% ▼
Zenji FM	55%	65%	+10% ▼
ZBC Radio	55%	69%	+14% ▼
Micheweni FM	48%	60%	+12% ▼
Safari FM	-	74%	- ▲

Mabadiliko makubwa yamejitokeza kwenye vyombo vya habari vilivyofanya vizuri kwenye eneo hili mwaka 2018. Magazeti yalishuhudia kushuka kwa “maoni mawili au zaidi” kutoka asilimia 32 hadi asilimia 13, na ongezeko kubwa la habari zisizokuwa na maoni (kutoka asilimia 40 hadi asilimia 64). Maendeleo yanayofanana na hayo yalifikwa na JamiiForums. Asilimia zao za habari zilizokuwa na “maoni 2 au zaidi” zilipungua kutoka asilimia 39 hadi asilimia 5 hata kama habari zao nyingi zilikuwa na angalau maoni (1) (asilimia 73). Redio za kitaifa zilibaki na alama zake (lakini kwa kiwango cha chini kwa mwaka 2018), wakati redio za mikoani na televisheni zilikuwa na habari chache zaidi zenye “maoni mawili au zaidi” kwa asilimia 10. Redio za mikoani zilishuhudia alama zao zikiporomoka kutoka asilimia 29 hadi asilimia 19 na televisheni kutoka asilimia 24 hadi asilimia 14. uhudia alama zao zikiporomoka kutoka asilimia 29 hadi asilimia 19 na televisheni kutoka asilimia 24 hadi asilimia 14.

## 2019: Maoni ndani ya habari na vipindi



### Taarifa za habari za redioni

Kwenye habari za redioni, asilimia 70 ya taarifa za habari zilizochunguzwa hazikuwasilisha maoni yoyote, asilimia 23 ziliwasilisha 1, na asilimia 7 maoni 2 au zaidi. Kiwango hiki cha ujumuishwaji wa maoni kwenye habari ni kidogo ikilinganishwa na cha mwaka 2018 ambapo asilimia 10 ya habari zilikuwa na maoni 2 au zaidi.

Hata hivyo, baadhi ya vituo vya redio viliwasilisha idadi kubwa ya maoni kuliko vituo vingine. Redio zilizoongoza katika kundi hili ni *Highlands FM*, *Clouds FM*, na *Dodoma FM*, ambazo nusu ya habari zao ziliwasilisha angalau maoni ya namna moja. Vituo hivyo pia viliongeza alama zake katika kipengele hiki ikilinganishwa na hali ilivyokuwa mwaka 2018. *TBC Taifa* iliingia kwenye orodha, hata hivyo ni kwa ongezeko la alama zake.

### Vipindi vya redio


Kwa wastani, vipindi vya redio huwasilisha kiwango kikubwa cha maoni zaidi kuliko kwenye habari. Kwa mwaka 2019, ni asilimia 45 tu ya vipindi vya redio

havikuwasilisha maoni yoyote. Hata hivyo, kulikuwa na asilimia 23 ya vipindi iliyowasilisha maoni 1, asilimia 33 ya vipindi iliwasilisha maoni 2 au zaidi. Hili linabainisha uimarikaji kidogo ukilinganisha na mwaka 2018 kwa sababu, kwa mwaka 2019 kulikuwa na habari chache kwa asilimia 3 ambazo hazikuwa na maoni ya aina yoyote.

Nyuma ya mwendelezo huu wa jumla kuna hali inayoonekana kinyume cha maendeleo haya miongoni mwa vituo vya redio. Vituo bora vya redio katika kuwasilisha angalau mtazamo mmoja kwenye vipindi vyao vilikuwa *Radio One*, *Safari FM*, *Pangani FM*, *Arusha 1 FM*, na *TBC Taifa*. Vituo vilivyofanya vizuri katika uwasilishaji wa “maoni mawili au zaidi” ni *Safari FM* (asilimia 61), *Pangani FM* (asilimia 60), *Radio One* (asilimia 48), *Highlands FM* (asilimia 43) na *Micheweni FM* (asilimia 42). *Clouds FM* (asilimia 15), *Zenj FM* na *ZBC Radio* (vyote asilimia 17) ndivyo vilivyofanya vibaya katika kipengele hiki.

Baadhi ya redio za mikoani ambazo zilifanya vizuri mwaka 2018 zilishuhudia ubora wao ukishuka kwa mwaka 2019. Redio hizi ni pamoja na *CG FM* (alama zake za maoni “2 na zaidi” ziliporomoka kutoka asilimia 73 hadi 35), *Dodoma FM* (kutoka asilimia 54 hadi 25), na *Micheweni FM* (kutoka asilimia 70 hadi 42). Kinyume chake, alama za *Radio One* zilipanda mno kutoka asilimia 22 hadi 48.

## 2019 Vipindi vya redio: Maoni 2 au zaidi



### Televisheni


Kwenye taarifa za habari za televisheni, vituo vingi havikujihusisha kabisa na uwasilishaji wa taarifa zenye maoni yoyote (kwa wastani wa asilimia 78), isipokuwa ZBC TV. Ikiwa asilimia 17 ya habari zake zikiwa na maoni (1), na asilimia 5 kubeba maoni 2 au zaidi, ni dhahiri kwamba ujumuishwaji wa maoni katika taarifa za habari umekuwa bidhaa adimu kwenye taarifa za habari za televisheni. Ni Azam TV pekee ambayo ilikuwa na asilimia 11 ya taarifa zake zikiwasilisha maoni 2 au zaidi.

Vipindi vya TV kwa ujumla huwasilisha maoni zaidi. Hata hivyo, asilimia 47 ya vipindi hivyo haviikuwa na maoni ya namna yoyote ile, sawa na ilivyo-bainika katika vipindi vya redio. Lakini kiwango hiki kinatofautiana miongoni mwa vituo vya TV. ZBC TV ilifanya vizuri zaidi kwa kuwa na idadi ndogo ya vipindi visivyokuwa na maoni, na idadi

kubwa ya vipindi vyenye maoni (1). Kinyume chake, Azam TV inaonekana kusita kujumuisha maoni kwenye vipindi ambapo asilimia 64 ya vipindi vyake havikubeba maoni yoyote. TBC 1 (asilimia 36) na ITV (asilimia 37) ndizo zilizokuwa na kiwango kikubwa cha vipindi vilivyokuwa na maoni 2 au zaidi ikifuatiwa na Azam TV (asilimia 21). ZBC TV iliingia kwenye rekodi kuwa miongoni mwa vituo ambavyo mara nyingi hutangaza habari zenye maoni (1) tu kwenye vipindi vyake.

Ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2018, idadi ya habari na vipindi vyenye maoni 2 au zaidi vimepungua sana. Kiwango hicho kilipungua kutoka asilimia 49 mwaka 2018 hadi asilimia 28 mwaka 2019. Vituo vya ITV na Azam TV ndivyo vilivyoonekana kudorora kutokana na kukosekana kwa vipindi vyenye maoni 2 au zaidi. Ikilinganishwa na 2018, ITV imeshuka kutoka asilimia 69 hadi 37, na Azam TV kutoka asilimia 46 hadi 21.


### 2019: Maoni kwenye habari za TV



## Magazeti

Changamoto ya kujumuisha maoni na misimamo kwenye maudhui inaonekana kuwa mbaya Zaidi kwenye magazeti. Idadi ya maoni na misimamo bayana imepungua. Ni idadi ndogo tu ya magazeti (au vyanzo vyake vya habari) ambayo inatoa maoni yao kwa uwazi kuhusu suala fulani.

### Maoni 2 au zaidi kwenye magazeti



Kwa wastani, asilimia 64 ya habari za gazetini hazikujumuisha maoni kabisa kwa mwaka 2019. Asilimia 23 pekee ndiyo ilikuwa na maoni (1), na asilimia 13 ilikuwa na maoni 2 au zaidi. Magazeti yaliyobainika kutokuwa na maoni ni Habari Leo (asilimia 83), na Daily News (asilimia 81), na The Guardian (asilimia 70). Mwanahalisi Online ilifanya vizuri kwa kuwa na asilimia 29 tu.

Magazeti yaliyoongoza katika kundi la vyombo vya habari vyenye maoni 2 au zaidi ni yale gazetini yanayotoka kila wiki yaani Raia Mwema (asilimia 32) na Jamhuri (asilimia 23), yakifuatiwa na Mwanahalisi (asilimia 20) na Mwananchi (asilimia 17). Magazeti yaliyokuwa na kiwango kidogo kabisa cha maoni 2 au zaidi ni Nipashe na Habari Leo (yote asilimia 5), na Daily News (asilimia 8).

Ikilinganishwa na 2018, kuna kiwango kikubwa cha kudorora kwa ubora wa uripoti. Kiwango cha habari zisizokuwa na maoni ya namna yoyote kiliongezeka kutoka asilimia 40 mwaka 2018 hadi asilimia 64 mwaka 2019. Sababu ni kwamba gazetini yote ambayo tayari yamo kwenye utafiti wa ubora wa mwaka 2018 alama zake zimeshuka kwenye eneo la uwasilishaji wa maoni anuwai. Kiwango kikubwa cha kudorora kilionekana katika gazetini la Mwananchi (lilipunguza utoaji wa maoni 2 au zaidi kutoka asilimia 48 hadi asilimia 17), Jamhuri (kutoka asilimia 40 hadi asilimia 23) na Nipashe (ilishuka hadi asilimia 5 kutoka asilimia 38).

### 4.7 Maoni kinzani

Uandishi bora wa habari ni sharti utoe habari yenye kuzingatia mizania. Hili hujumuisha uwasilishaji wa mitazamo ya namna zaidi ya moja na ikiwezekana kutafuta na kuwasilisha maoni kinzani ili kuifanya hadhira ielewe upande wa pili unasemaje. Jambo hili linafanya kuwe na tafakuri yenye usawa katika kutoa mawazo kuhusiana na suala linaloandikwa.


Takwimu za mwaka 2019 zinaonesha kuwa idadi ya habari zenye maoni 2 au zaidi ilipungua ikilinganishwa na idadi ya mwaka 2018. Kwa hivyo, idadi ya maoni kinzani nayo ilipungua vile vile kwa kuwa habari au kipindi kinahitaji angalau mitazamo miwili ambayo kwa dhati yake inakinzana.

### Vyombo vyote vya habari

Mwaka 2019, idadi ya maoni kinzani ilikuwa ndogo sana. Kwa wastani, ni asilimia 2.8 tu ya kazi zilizo-chambuliwa ndiyo ilikuwa na maoni kinzani. Jamii-Forums ilikuwa na asilimia 5, ikifuatiwa na magazeti yaliyokuwa na asilimia 3.5 ya maoni. Kwa kuwa idadi ya maoni ilikuwa ndogo mno, ni kama hakukuwa kabisa na maoni kinzani ya namna yoyote. Mwaka 2018 hali ilikuwa nzuri kiasi, lakini ilijitokeza katika *JamiiForums* na magazeti. Redio na TV zilikuwa na kiwango kidogo sana cha maoni kinzani.



## 2019 : Maoni kinzani



### Redio

Kwenye taarifa za habari za redioni ni nadra sana kupata maoni kinzani. Kwa wastani jambo hili lilijitokeza kwa asilimia 1 tu. Ni *Highlands FM* (asilimia 6) na *Radio One* (asilimia 5) ndivyo vyombo pekee wakati fulani viliwasilisha habari zenye maoni kinzani. Katika vipindi vya redio, *Pangani FM* (asilimia 27) inaongoza katika kuwasilisha maoni ya namna hii, ikifuatiwa na *Safari FM* (asilimia 11) na *CG FM* (asilimia 8). Redio zilizobaki zilikuwa na ama asilimia 0 au chini ya asilimia 2.

### Televisheni

Pia ni nadra kuwa na maoni kinzani kwenye televisheni. Hata 'kituo bora' *ZBC TV* kilikuwa na kiwango kidogo cha maoni kinzani (chini ya asilimia 5). *ITV* ilikuwa na habari moja tu yenye maoni kinzani. *TBC 1* na *Azam TV* hazikuwa na maoni kinzani yoyote. Hali ilikuwa nzuri kiasi mwaka 2018, ingawa ilikuwa kwa *Azam TV* peke yake (asilimia 7.5).

### Jedwali 6: Habari zenye kuikosoa Serikali

	Idadi	Asilimia
Magazeti	31	4%
Redio za Kitaifa	1	0.3%
Redio za Mikoani	5	1%
TV	0	0%
JamiiForums	25	31%

### Magazeti

Mwaka 2019, ni magazeti ya *Mwanahalisi* (asilimia 13), *Jamhuri* (asilimia 7), *Mwananchi* na *Raia Mwema* (yote asilimia 5) tu ndiyo yalikuwa na angalau baadhi ya habari zenye maoni kinzani. Kiulinganishi, kiwango hiki cha ufanisi bado kinahitaji kuongezwa ingawa hakijabore-shwa sana tangu mwaka 2018. Kwa magazeti ambayo yalikuwa sehemu ya utafiti wa 2018, utendaji wao wa jumla katika kipengele hiki umeshuka.

### 4.8 Maoni yaliyoikosoa Serikali

Tafiti hii inachunguza ikiwa baadhi ya maoni yaliyomo kwenye habari yanaikosoa serikali au la.

Maoni yaliyoikosoa serikali yalikuwa machache sana. Mara nyingi magazeti yalipaza sauti za kiukosoaji, lakini hili limebainika kwa asilimia 4 tu ya habari zote zilizochunguzwa. *Jamii-Forums* ndiyo inayotoa maoni yenye kiukosoa serikali kwa asilimia 31 tu ya taarifa zake zilizochunguzwa. Matokeo kwenye redio za mikoani ni mbaya zaidi.

## Redio

Ni redio chache tu zilithubutu kuikosoa serikali. Hata hivyo, hakuna kituo chochote cha redio kilichokosoa serikali zaidi ya mara moja.

## Televisheni

Hakukuwa na habari yoyote kwenye televisheni iliyokuwa na maoni yaliyoikosoa serikali.

## Magazeti

Ni habari chache tu za kwenye magazeti ziliikosoa serikali mwaka 2019. Kwa maneno mengine, habari zilizoikosoa serikali zilichapishwa kwa nadra sana. Magazeti ya *Mwanahalisi*, *The Citizen* na *Mwananchi* yaliongoza kuchapisha habari hizi, lakini ilikuwa kwa asilimia 10 tu ya habari zake zote au chini ya hapo. Hali hii ni sawa na ilivyokuwa mwaka 2018.

## 4.9 Haki ya kujibu tuhuma

Habari inahitaji kuzingatia haki ya kujibu tuhuma ikiwa mtu au taasisi fulani inatuhumiwa kufanya uovu. Katika mazingira hayo, mtu anayetuhumiwa anahitaji kupatiwa fursa ya kujibu tuhuma zinazomkabili. Haki hii imechunguzwa katika habari zote, isipokuwa habari zilizohusiana na makosa ya jinai au kesi mahakamani.

## Vyombo vyote vya habari

Haki ya kujibu tuhuma ilibainika kwenye asilimia 31 tu kwa habari zilizochunguzwa. Jambo hili linaonekana kuwa ni changamoto kubwa ya kimaadili kwa vyombo vya habari nchini Tanzania. Redio za kitaifa zilikuwa na kiwango kidogo kabisa cha ufanisi katika jambo hili. Magazeti yalifanya vizuri ingawa kwa kiwango kidogo sana. Kiwango cha uzingatiaji wa haki ya watuhumiwa kujibu tuhuma dhidi yao kilikuwa kikubwa mwaka 2018 (42 asilimia), ingawa kiwango hiki hakikubaliki kiweledi.

## Redio

Kulikuwa na visa vichache mno vilivyohusiana na suala la haki ya kujibu au kuwasaili watuhumiwa (asilimia 21) katika sampuli yote ya redio zilizochunguzwa na idadi kubwa ya redio ilikuwa na kisa kimoja au viwili. Chombo kilichofanya vizuri zaidi ni *Zenj FM* (kisa 1 kilichohusisha haki ya kujibu), *Safari FM* (visa 3, asilimia 67), na *Radio One* na *Micheweni FM* (zote zikiwa na visa 2, asilimia 50).

## Televisheni

Hali inayofanana na hiyo pia inajidhihirisha kwenye TV. Vyombo vilivyofanya vizuri zaidi ni *Azam TV* (kisa 1, asilimia 100) na *ITV* (visa 4, asilimia 50). *TBC 1* (visa 4, asilimia 0) na vyombo vingine vilifanya vibaya. Ikilinganishwa na mwaka 2018, ni dhahiri kuwa kiwango cha ufanisi cha *ITV* na *Azam TV* kimeongezeka kuhusiana na kutoa haki kwa watuhumiwa kujibu tuhuma dhidi yao.

## Magazeti

Kulikuwa na habari nyingi katika magazeti zilizowapa watuhumiwa fursa ya kujieleza. *Daily News* na *Zanzibar Leo* zilifanya vizuri sana (visa 1-2, asilimia 100). Kwa vyombo vilivyokuwa na idadi kubwa ya visa (zaidi ya 10), *Mwananchi* imefanya vizuri kwa kuwa na asilimia 47 ya visa ambapo watuhumiwa walipewa fursa ya kujibu, *Mwanahalisi* ilipata kiwango kidogo kwa kuwa na asilimia 27 peke yake. *Mwananchi* (asilimia 73) na *Jamhuri* (asilimia 64) ikiwa zimefanya vizuri zaidi mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2019.

## 4.10 Ujumuishaji wa kiini kikuu cha habari


Utafiti huu huangalia kama habari ina kiini kikuu cha taarifa. Baada ya hapo, habari hiyo inafanywa tathmini ili kuona ikiwa inaelezea kiini cha tatizo au suala linalojadiliwa kwenye habari (siyo sababu nyingine za jambo jingine).

Ujumuishaji wa kiini cha suala husika una mchango chanya wa kuisaidia hadhira kuelewa vyema matukio na masuala yanayowasilishwa katika vyombo vya habari.

## Vyombo vyote vya habari

Kwa wastani, asilimia 23.5 ya habari hujumuisha kiini cha habari husika. Hii ni sawa na ilivyokuwa mwaka 2018. Hata hivyo, kuna tofauti kadhaa miongoni mwa aina mbalimbali za vyombo vya habari. Bado magazeti yanaongoza kwa kuwa na wastani wa asilimia 27 ingawa hiyo ni sawa na kupungua kwa asilimia 10 kutoka kiwango cha mwaka 2018. Redio za kitaifa na za mikoani zilikuwa na wastani wa asilimia 18 na 23, sawa na ongezeko la asilimia 2 na 3 mtawalia. TV zimekuwa na msimamo uleule wa asilimia 25. JamiiForum ilikuwa na asilimia 10, hali inayoonesha kwamba asilimia ndogo ya midahalo katika jukwaa hilo hujumuisha kiini cha masuala yanayojadiliwa.

## 2019: Sababu za kuandikwa kwa habari




### Taarifa za habari redioni

Kwa ujumla, kiwango cha uelezaji wa kiini katika taarifa za habari redioni ni kidogo. Kwa mwaka 2019 na 2018, ni asilimia 12 tu ya habari zilifanya hivyo. Hata hivyo, kuna maendeleo mapya kwenye baadi ya vituo vya redio. Redio iliyofanya vizuri zaidi ilikuwa *Highlands FM* (asilimia 30), ikifuatiwa na *Arusha 1 FM*, *Dodoma FM* na *Radio One* (zote zilikuwa na asilimia 18). Hii ilifuatiwa na *ZBC Radio* (asilimia 16), na *Zenj FM* na *CG FM* zote zilikuwa na wastani wa asilimia 14. Redio zilizofanya vibaya zaidi zilikuwa *Radio Free Africa* (asilimia 3), *Clouds FM* na *Micheweni FM* (zote zilikuwa na asilimia 4).

Ikilinganishwa na 2018, *Clouds FM* imeshuka sana (asilimia 16 zimepungua). *Pangani FM* pia imeshuka. Kwa upande mwingine, *Highlands FM* na *Arusha 1 FM* zimeendelea kuimarika, zote zikiwa zimepanda kutoka sifuri hadi kufikia asilimia 30 na asilimia 18 mtawalia.

## Sababu za kuripotiwa habari kwenye taarifa za habari za redio




### Vipindi vya redio

Kwenye vipindi vya redio, kuna ongezeko la uelezaji wa kiini cha masuala yanayohusika. Kwa wastani, hili lilionekana kwa asilimia 33 ya maudhui yote kwa mwaka 2019, ikilinganishwa na asilimia 24 mwaka 2018, ikiwa ni ongezeko la wastani wa asilimia 9. Vyombo vilivyoongoza kwa ubora katika kipengele hiki vilikuwa *Micheweni FM* (asilimia 75), ikifuatiwa na *Radio One* (asilimia 59), *Dodoma FM* (asilimia 50), *Pangani FM* (asilimia 40) na *CG FM* (asilimia 38). Redio zilizofanya vibaya zaidi zilikuwa *Clouds FM* (asilimia 6), *Highlands FM* (asilimia 14), *ZBC Radio* na *Safari FM* (zote zikiwa na asilimia 17). Pamoja na maendeleo chanya, hali hii inaweza kuboreshwa zaidi hasa kwa kuwa vipindi virefu vya redio hutoa nafasi ya kuihabarisha jamii kuhusu kiini cha suala husika.

Tunapoyaangalia maendeleo yaliyopatikana kati ya 2018 na 2019, ni dhahiri kuwa TBC Taifa, Radio Free Africa, *Radio One* na *Micheweni FM* zimeimarika zaidi. Baadhi ya vituo vya redio kama vile *CG FM*, *Highlands FM*, *Arusha 1 FM* na *Zenj FM* zimebaki katika hatua ileile ya awali, au zimeimarika kidogo mno. Hata hivyo, kiwango cha uelezaji wa kiini cha tatizo kwa redio za *Clouds FM* na *ZBC Redio* kimepungua kwa mwaka 2019.

## 2019: Sababu za kuripotiwa habari kwenye vipindi vya redio




## Televisheni

Katika habari za televisheni, ujumuishwaji wa kiini cha taarifa umekuwa mdogo sana. Ni ZBC pekee ambayo habari zake zina zaidi ya asilimia 10 ikielezea kiini cha taarifa husika. Kinyume chake, vipindi vya TV vinajitahidi kuangazia kiini cha taarifa ukilinganisha na taarifa za habari. Kituo cha ITV (asilimia 70) kinaongoza, kikifuatiwa na Azam TV (asilimia 64) na

TBC 1 (asilimia 64). Kituo cha ZBC TV kiko nyuma kikiwa na asilimia 20.

Ikilinganishwa na mwaka 2018, vipindi vya TV vimeimarika kwa ujumla wake kwa asilimia 13 kwa sababu uimara uliooneshwa na TBC1 (asilimia 64 dhidi ya 12 mwaka 2018), ITV (ongezeko la asilimia 13) na Azam TV (ongezeko la asilimia 14).

## 2019: Sababu za kuandikwa habari kwenye TV




## Magazeti

Uelezeaji wa kiini cha habari katika magazeti ulikuwa asilimia 27, kiwango ambacho kimeshuka kwa pointi asilimia 10 kutoka kwenye takwimu za mwaka 2018. Magazeti yaliyofanya vizuri zaidi kwa mwaka 2019 ni Raia Mwema (asilimia 45) likifuatiwa na *Nipashe* (asilimia 40), *Mwananchi na The Guardian* (kila moja likiwa na asilimia 32). Yaliyokuwa nyuma ni *Daily News* (asilimia 13), *Habari Leo* (asilimia 20), na *Jamhuri* (asilimia 23). Kwa magazeti mengine kama *Zanzibar Leo* (asilimia 25), *The Citizen* (asilimia 25) na

*Mwanahalisi Online* (asilimia 26), ubora wao ulikuwa karibu na wastani.

Kwa kuangalia maendeleo kati ya mwaka 2018 na 2019, kushuka kwa gazeti la *Jamhuri* ni kwa kiwango cha juu. Gazeti hilo lilishuka kutoka asilimia 54 mwaka 2018 mpaka asilimia 23 mwaka 2019. Lilifanya vizuri sana mwaka 2018. *Daily News* limeporomoka kwa kiwango kikubwa pia kutoka asilimia 45 mpaka 13. *The Citizen* (asilimia 25) na *Mwananchi* (asilimia 31) yameendelea kubaki kwenye nafasi zilezile za mwaka 2018. Alama za gazeti la *Nipashe* ziliongezeka kwa asilimia 9.

### 2019 Magazeti: Sababu kubwa




#### 4.11 Uwekaji wa takwimu kwenye muktadha mzuri

Utumiaji wa takwimu kwenye kazi ya kihabari ni namna nzuri ya kufanya matukio yawe thabiti. Muhimu zaidi ni kwa takwimu hizo kufafanuliwa vizuri kwa kuizweka katika muktadha fulani, yaani zilinganishwe na kitu ambacho msomaji au msikilizaji anakielewa vizuri.

#### Vyombo vyote vya habari

Mwaka 2019, redio za mikoani ziliweka takwimu katika muktadha kwa asilimia 60, zikifuatiwa na redio za kitaifa (asilimia 46) na magazeti (asilimia 36). Vituo vya TV vilifanya hivyo kwa asilimia 25. Ubora ulimari-ka zaidi ukilinganisha na mwaka 2018 kwa kuwa wastani kwa mwaka 2019 (asilimia 42) ulikuwa wa juu zaidi ukilinganisha na wastani wa asilimia 25 wa mwaka uliotangulia.

## 2019: Matumizi ya takwimu kwenye habari



### Redio

Kwenye redio, ushughulikiaji wa takwimu kwa kiasi kikubwa ulikuwa mzuri hususani miongoni mwa vituo vya redio za mikoani. Vituo vya *Pangani FM, Arusha 1 FM, Zenji FM, na Micheweni FM* - vyote vilikuwa na asilimia 67 ya ripoti zao zilizoweka takwimu katika muktadha mzuri. Kituo cha mwisho kilikuwa *TBC Taifa* chenye asilimia 25 pekee.

Vituo kumi vya redio vilifanya vizuri mwaka 2019 ukilinganisha na mwaka 2018. Kituo kilichofanya vizuri zaidi katika kipengele hiki ni *CG FM* chenye asilimia 54.

### Televisheni

Vituo vya televisheni havifanyi vizuri katika kipengele hiki. Mara nyingi, vimesimama kwenye wastani wa asilimia 25 katika kipengele hiki. Kituo cha *ZBC TV* (asilimia 32) kiliongoza na kufuatiwa na kituo cha *Azam TV* (asilimia 28), na *ITV* (asilimia 22). *Ayo TV* ilikuwa na asilimia 0. Hata hivyo, ukilinganisha na 2018, hakuna mabadiliko makubwa yaliyotokea isipokuwa kwa kituo cha *ITV*, ambacho kilikuwa chini mwaka 2018, kimeimarika sana. *Ayo TV* imeanguka vibaya sana mpaka asilimia 0.

### Magazeti

Katika magazeti, asilimia 36 ya takwimu zinawekwa katika muktadha mzuri. Hata hivyo, kuna

tofauti kubwa baina ya magazeti mbalimbali. Gazeti la *Raia Mwema* (asilimia 54) linaongoza, likifuatiwa na *Habari Leo, Nipashe, Mwananchi, Zanzibar Leo* na *Jamhuri*, ambayo huweka takwimu katika muktadha mzuri kwa asilimia kati ya 45 na 50. Kuna pengo kubwa kati ya magazeti yanayoshika nafasi ya chini na yale yanayoshika nafasi ya juu. *The Guardian* (asilimia 28), *The Citizen* (asilimia 26), huku *Daily News* ikiwa na asilimia 16 na *Mwanahalisi* asilimia 13.

Ikilinganishwa na mwaka 2018, kuna maboresho ya jumla. Ni *Daily News* pekee ndilo lililofanya vibaya. Magazeti ya *The Citizen* na *The Guardian* yamebaki katika kiwango kilekile ingawa mengine yameimarika mno.

### 4.12 Miundo ya kiuandishi katika habari

Habari yoyote ya kihabari lazima iwe na uwiano ili hadhira ya chombo cha habari iweze kuelewa kwa urahisi. Kwa hiyo, inapaswa iwe wazi na yenye uhusiano wa kimantiki ili sehemu mbalimbali za habari hiyo ziwe na upatanifu.

### Vyombo vya habari vyote

Mwaka 2019, asilimia 54 ya kazi za habari zilikuwa na muundo mzuri sana, na asilimia 42 zilionekana kuwa na miundo inayoridhisha. Ni asilimia 4 tu ya kazi zilizochunguzwa ndizo zilizokuwa na changamoto katika miundo yake. Redio za kitaifa zilikuwa na asilimia 61 ya kazi zao zilizokuwa na

muundo mzuri. Televisheni zikiwa na asilimia 60, zilifanya vizuri zaidi ya wastani. Magazeti yalifanya vibaya yakiwa na asilimia 47.

Magazeti hayakufanya vizuri sana mwaka 2019 kutokana na kupungua makala zenye ubora wa muundo kutoka asilimia 57 mpaka asilimia 47. Kwenye redio za kitaifa, takwimu ziliongezeka kutoka asilimia 49 mpaka asilimia 61.

## Redio

Redio zilikuwa na asilimia 57 ya kazi zenye miundo mizuri. Redio zilizofanya vizuri katika kipengele hiki ni *Clouds FM* (asilimia 74), *TBC Taifa* (asilimia 68), *Micheweni FM* (asilimia 65) na *Radio Free Africa* (asilimia 61). Redio zilizoshika mkia zilikuwa *ZBC Radio* (asilimia 47), na *Highlands FM* (asilimia 45). Ukilinganisha na mwaka 2018, ubora wa muundo umeimarika katika Redio. *TBC Taifa* na *Clouds FM* zilikuwa na mabadiliko yaliyoonekana dhahiri katika kipengele hiki.

## Televisheni

Kwa wastani, alama za TV, asilimia 60, katika muundo mzuri wKwa wastani, alama za TV, asilimia 60, katika muundo mzuri wa kiuandishi ni za juu zaidi ya redio. *ZBC TV* ilikuwa na alama za juu kuliko televisheni zote ikiwa na asilimia 71, ikifuatiwa na *ITV* (asilimia 70), na *TBC 1* (asilimia 66). *Ayo TV* ilifanya vibaya ikiwa na asilimia 18. Hata hivyo, ubora ulishuka kwa asilimia 4 kutoka mwaka 2018.

## Magazeti

Mwaka 2019, magazeti yalikuwa na asilimia 47 tu ya makala zake zenye miundo mizuri. Ubora ulishuka ukilinganisha na mwaka 2018. Magazeti yaliyofanya vizuri yalikuwa *Mwanahalisi* (asilimia 79) na *Mwananchi* (asilimia 58). Yaliyokuwa nafasi ya chini ni *Daily News* (asilimia 29), na *Jamhuri*, *The Citizen*, na *Nipasha* (yote yakiwa na asilimia 39). Kwa wastani, kulikuwa na anguko la pointi za asilimia 10. Magazeti yaliyoathirika ni pamoja na *The Citizen* (pungufu kwa 19%), *Daily News* (pungufu kwa 24%), *Zanzibar Leo* (pungufu kwa 17%) na *Jamhuri* (pungufu kwa 30%)., *Daily News*, *Zanzibar Leo* na *Jamhuri*.

### 4.13 Usuli wa habari

Kazi ya kihabari iliyo nzuri inatoa taarifa ya usuli wa kihistoria ya suala au tatizo katika habari ili kuiwezesha hadhira kuelewa usuli wa suala lililopo.


Mwaka 2019, urejeleaji wa usuli wa kihistoria ulifanyika kwa nadra, lakini ulikuwa bora ukilinganisha na mwaka 2018. Kwa wastani, asilimia 11 ya habari zilikuwa na aya/sentensi mbili au zaidi kuhusu usuli wa kihistoria wa tukio au suala linaloelezwa. Hiyo ni asilimia 2 zaidi kwa vyombo vyote vya habari. Magazeti yalikuwa na asilimia 15 ya urejeleaji wa usuli wa kihistoria (pungufu ya asilimia 2), redio za kitaifa asilimia 11 (ongezeko la asilimia 8), redio za mikoani asilimia 9 (ongezeko la asilimia 1) na TV zenye asilimia 7 pekee (pungufu ya asilimia 6).

### 4.14 Habari kutoka miji mikubwa na midogo

Kipengele hiki kinatazama iwapo habari inatokea katika miji mikubwa iliyoko Tanzania bara na Zanzibar (Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Mjini Magharibi na Kusini Pemba) au katika miji midogo na maeneo ya vijijini.

Mwaka 2019, matumizi ya habari kutoka miji mikubwa na midogo yalibadilika kidogo. Kwa wastani, maeneo ya vijijini yalielezwa kwa kiasi kidogo ukilinganisha na mwaka 2018 (pungufu ya asilimia 5). Vituo vya redio za mikoani vilipunguza kuelezea masuala ya maeneo ya vijijini ukilinganisha na aina nyingine ya vyombo vya habari. Televisheni zilikuwa thabiti kwenye nafasi ileile.


## 2019: Habari za mijini na nje ya miji



### 4.15 Habari za mikoani na kitaifa

Tafiti hii ilitazama iwapo habari inaelezea suala pana lenye umuhimu wa kitaifa au iwapo ni mahususi kwa eneo fulani kama inavyooneshwa katika jedwali.

### Habari za kitaifa na za mikoani



### 4.2 Kielezo cha Ubora wa Vyombo vya Habari

Kielezo cha ubora wa vyombo vya habari kinatoa muhtasari wa mafanikio katika vipengele tofauti vya ubora katika kielezo kimoja. Hata hivyo, mwaka 2019 kigezo kipya kiliongezwa kwenye kielezo ambacho ni "uwekaji wa takwimu katika muktadha mzuri". Hivyo kielezo hiki kimejikita katika vigezo vya ubora 10.


### Jedwali 7 : Kielezo cha Ubora wa Vyombo vya Habari 2018 - 2019

	Idadi	Asilimia
Magazeti	31	4%
Redio za Kitaifa	1	0.3%
Redio za Mikoani	5	1%
TV	0	0%
JamiiForums	25	31%



Vyombo vya habari vitano vinavyoongoza kwa mwaka 2019 ni Micheweni FM (iliyofanya vizuri zaidi), ikifuatiwa na Radio One, Raia Mwema, Mwananchi zilizokuwa na ubora unaolingana na kisha gazeti la Jamhuri. Vyombo vya habari vilivyoshika nafasi ya chini ni ZBC TV, Clouds FM, TBC 1, Habari Leo, TBC Taifa, The Guardian na Ayo TV.

## Kiwango cha ubora cha chombo cha habari mwaka 2019



## 5.0 UBORA WA MAUDHUI NA MTAZAMO WA WADAU

Katika uzinduzi wa ripoti ya mwaka 2018, baadhi ya washiriki walibainisha kuwa kulikuwa na uhitaji wa kupanua lengo la utafiti zaidi ya uchambuzi wa maudhui. Swali mojawapo muhimu lililoulizwa lilikuwa: “Je tunafahamu, kwa kuzingatia uzoefu wa vyumba vya habari, kwa nini ubora wa vyombo vya habari unaporomoka? Swali hili lilizaa kipengele ambacho kinalenga kuitikia maoni ya wahariri na wadau kuhusu ubora wa uripoti wa vyombo vya habari nchini Tanzania.

Kwa jumla, wahariri 10, wawakilishi 2 kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali ya habari, na wahadhiri wa taaluma ya uandishi wa habari 3 walihojiwa. Maswali yaliyoulizwa yaliwekwa katika makundi matatu: mazingira ya kisiasa, mazingira ya kiuchumi, na mazingira ya vyumba vya habari na uhusiano wake na ubora wa uripoti wa vyombo vya habari.

Wahojiwa wengi walidai kuwa mazingira ya kisiasa na kiuchumi nchini yamekuwa changamoto kubwa kwa jukumu la vyombo vya habari kumulika utendaji kazi wa serikali. Wanayaona mazingira ya sasa ya kisiasa kuwa kikwazo cha kupata vyombo vya habari vilivyo huru, vinavyokosoa na vinavyojitegemea. Maneno ‘hofu ya mazingira ya sasa ya kisiasa’ yalisemwa karibu na wahariri wote waliohojiwa. Mhariri Mtendaji Mwandamizi mmoja alitoa muhtasari wa mazingira ya sasa ya kisiasa na uendeshaji wa vyombo vya habari kama ifuatavyo:

*“Wahariri wanaona hawako salama kuchapisha habari za ndani za kisiasa kama ilivyokuwa kabla. Kuna hofu katika vyumba vya habari linapokuja suala la kuandika habari hizi. Hofu hii imetanda kwa wahusika wote [katika vyumba vya habari] kuanzia watendaji wakuu, wahariri mpaka kwa waandishi. Jambo hili, kwa kiasi fulani, linaeleza kwa nini magazeti yote ya kisiasa ama yalifungiwa au kupigwa marufuku.”*

Mhariri mwingine alitoa maoni kama hayo. Alibainisha kuwa kufungiwa kwa magazeti kunatoa onyo kali kwa wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri na waandishi. Jambo hili, mhojiwa aliongeza, “limepanda hofu na mashaka

katika vyombo vya habari kwa wahariri kuamua kuchapisha habari salama na zisizo za kisiasa.”

Wakitoa maoni zaidi kuhusu namna ambavyo habari za kisiasa zinavyowekwa kando katika vyumba vya habari, mhariri mmoja aliziita habari za kisiasa ‘mengineyo’ katika orodha ya habari zinazopewa kipaumbele.

*“Habari hizi za kisiasa haziko tena katika orodha yetu ya habari tatu za juu. Ikitokea tunazichapisha, basi tunaripoti katika hali chapwa zaidi kuliko ukosoaji. Kwa mtazamo wa kibiashara, na kwa kuzingatia hali ya sasa ya kisiasa ambayo hairuhusu uripoti unaokosoa, haileti maana kibiashara kufuatilia habari hizi. Ni bora tuendelee kubaki sokoni kuliko kufungiwa au kupigwa marufuku. Jambo hili ni baya kwa umma... lakini nadhani hakuna namna.”*

Kwa mujibu wa wahojiwa, mazingira ya sasa ya kisiasa yamesababisha hali ya kujidhibiti ndani na nje ya vyumba vya habari. Wahojiwa wengi wanaona kuwa wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri, waandishi na hata umma kwa ujumla, sasa wanajidhibiti kutoa maoni yao. Walibainisha kuwa, watu wanasita kutoa maoni yao kwa uwazi, hususani yale yanayoonekana kuwa ya ukosoaji kwa serikali. Suala hili linajidhihirisha katika ngazi za mikoa (yenye vyombo vya habari vya kimkoa na vya kijamii) na ngazi ya kitaifa (vyombo vya habari vya kitaifa).

Mhariri anayefanya kazi katika chombo kimojawapo cha kitaifa alifafanua changamoto za kupata maoni ya kukosoa kutoka kwa wataalamu na watu wenye elimu kama ifuatavyo:

*“... Wakati mwingine, tunalazimika kuacha habari kubwa kwa sababu hatupati watu sahihi wa kutueleza wanachofikiria au kutupatia maoni ya kitaalamu. Inakatisha tamaa tunapowapigia wataalamu kwa ajili ya kupata maoni yao... na wanapotambua kuwa mada tunazozifuatilia ni za kuikosoa serikali, watatoa udhuru ama kwa kusema watatupigia au wako mkutanoni. Tunapowapigia kwa mara nyingine, hawapokei simu. Katika vyumba vya habari, tunatafsiri jambo hili kama ‘Siko tayari kuzungumza.’ Na huo ndio mwisho wake.”*

Wahojiwa kutoka vyuoni na asasi zinazojishughulisha na masuala ya habari nchini wanaunga mkono maoni hayo wakibainisha kuwa mazingira ya sasa ya kisiasa kwa hakika yanafanya kazi ya waandishi kuwa ngumu zaidi, na hivyo kuwalazimisha waandishi kuachana na baadhi ya masuala. Mhojiwa mmojawapo alibainisha: "Nimekuwa nikifundisha waandishi kwa miaka mingi sasa, na mojawapo ya malalamiko yao yamekuwa kubanwa kwa mazingira ya vyombo vya habari ambayo kwayo waandishi hawako tena huru kuchunguza na kuchapisha habari zinazoonekana kukosoa serikali."

Mhariri wa gazeti mojawapo alitoa mtazamo tofauti. Anasema kuwa waandishi kujizua kuandika habari fulani si jambo geni katika vyumba vya habari. Wahariri wakati mwingine huchapisha habari zisizo na upana wa weledi. Pengo hili la kiweledi, mhojiwa alibainisha, linasababisha serikali kutumia sheria zilizopo kuadhibu au kuviwekea vikwazo vyombo vya habari. "Kuna mazingira ambayo vyombo vya habari vinachapisha habari ambazo ama zimeegemea upande mmoja au hazina uthibitisho na bado zinakosoa serikali. Chombo cha habari kinapofungiwa au kupigwa marufuku kwa sababu ya tatizo la kiweledi, unasikia vilio kila kona. Kwetu sisi wanahabari, kuna masuala ya kiweledi tunayopaswa kuyashughulikia kwa dhati."

Mhariri mwingine alibainisha kuwa kuna ongezeko la makosa ya kitaaluma miongoni mwa waandishi wa habari. "Si haki kila wakati kuilaumu serikali. Kuna matukio ambayo wahariri wamechapisha habari zinazotia mashaka... Na sisi wahariri tunapozipima, tunaambizana kuwa habari hizo hazikupaswa kuchapishwa."

Ingawa wahojiwa wote wanakubaliana kuhusu hitaji la kuongeza weledi, baadhi walihoji hatua za kiupendeleo za serikali katika kushughulikia mwenendo wa kiweledi usioridhisha. "Inaonekana kuna magazeti nchini yako radhi kuuangamiza weledi. Tumeona baadhi ya magazeti...yanachapisha habari za kupika na zinazoegemea upande mmoja kwa zaidi ya mwaka na hakuna aliyewafungia au kuwapiga marufuku."

Zaidi ya mazingira ya kisiasa, ubora wa uripoti umeathiriwa na hali ya sasa ya kiuchumi. Kutokana na mapato ya matangazo kuporomoka, vyombo vya habari viko katika 'hali ya kupambana kuendelea kuwapo'. Jambo hili, kwa mujibu wa wahojiwa, linaathiri uendeshaji kwa namna

mbalimbali. Vyombo vya habari vinapata shida kutafuta habari zao wenyewe, hivyo huishia kutegemea habari za matukio. Wengi sasa hawawezi kufanya habari za uchunguzi. Haviwezi kuchimba undani wa habari, ukiachilia mbali kuzalisha vipindi vya nje ya studio n.k. Mambo haya yanapokuwa magumu kufanikiwa, ubora wa uripoti wa habari unakuwa matatani.

Pia kuna changamoto ambazo ziko ndani ya vyumba vya habari. Mahojiano na wahariri yalithibitisha changamoto kuu nne ndani ya vyumba vya habari ambazo zinaathiri ubora wa uripoti wa habari. Changamoto hizo ni kutokutii kanuni za uandishi, wahariri wasio na uzoefu, kukosekana kwa waandishi wenye sifa na kuzidi kwa majukumu miongoni mwa waandishi.

Kutozingatia kanuni na taratibu zilizowekwa kulithibitishwa na wahariri wengi kuwa ni mojawapo ya sababu inayochangia kuwa na uduni katika uripoti wa habari. Ingawa inakubalika kuwa habari inapaswa kuwa na angalau vyanzo viwili, baadhi ya wahariri wanaridhika na habari yenye chanzo kimoja. Aidha, baadhi ya wahariri huridhika kwa habari kuwa na mtazamo mmoja ingawa inatambulika kuwa habari nzuri inapaswa kuwa na mtazamo zaidi ya mmoja. Wakati ni wajibu wa kiweledi kuhakikisha kunakuwepo 'haki ya kujibu tuhuma' kwa mtuhumiwa, baadhi ya wahariri wanaruhusu kuchapishwa kwa habari bila kumpatia mtuhumiwa 'haki ya kujibu' tuhuma.

Mapitio ya sera kadhaa za uhariri nchini yanaonesha kuwa kuna matakwa kadhaa ya kiweledi ndani ya sera hizo. Hata hivyo, hakuna muunganiko kati ya matakwa, matarajio na hali halisi ilivyo. Hiki ndicho wahojiwa wanachokiita 'kutokutii kanuni'. "Wahariri na waandishi wa habari wanajua kinachotakiwa, lakini huamua kutotii matakwa ya kiweledi na kiuhariri," anasema.

Kuna mtazamo kutoka kwa waandishi na wahariri wakongwe kuwa sasa madawati ya habari yanasimamiwa na wahariri vijana wasio na uzoefu. Hawa, wanadai, ndio wanaochangia hali ya sasa ya uripoti wa habari. Ingawa ni kweli kuna ongezeko dhahiri katika idadi ya wahariri vijana - sawa na ongezeko la idadi ya mameneja vijana katika sekta nyingine - matokeo ya utafiti huu hayaungi mkono mtazamo huu. Vyombo vya habari vinavyoongozwa na wahariri vijana hususani vituo vya redio za mikoani vimefanya vizuri kama vile vinavyoongozwa na wahariri wakongwe au wazoefu.

Kukosekana kwa waandishi wenye sifa pia kulitajwa kuwa jambo linalochangia hali ya sasa ya uripoti wa vyombo vya habari. Baadhi ya wahariri walilalamikia ubora wa waandishi wa hitimu, wakidai kuwa hawawezi kukidhi ubora unaotarajiwa kutoka kwao. Wahitimu wanaonekana kukosa ujuzi wa kufanya utafiti na stadi za uandishi pamoja na uwezo wa kuzalisha habari nzuri. Mhariri mmoja alisema:

*"... (W)ahitimu wa uandishi wa habari wanakosa ujuzi wa kiuandishi. Ni katika lugha zote za Kiswahili na Kiingereza, ingawa tatizo kubwa liko zaidi kwenye Kiingereza. Hapa simaanishi kuandika habari isiyo na makosa ya kiuandishi, bali uwezo wa kuandika habari inayoharirika. Ninaona jambo hili kuwa mojawapo ya changamoto ambazo wahariri wengi wanakumbana nazo. Hata hivyo, ninapaswa kusema kuwa sisi [wahariri] hatuwafundishi na kuwashauri waandishi hawa vijana. Ni vyumba vya habari vichache sana, pengine kimoja au viwili, ndivyo vina wahariri maalumu wenye jukumu la kusimamia mafunzo ya ndani. Kwangu, jambo hili ni muhimu... tunahitaji kuyapa kipaumbele mafunzo kazini kwa kuwa na kozi zilizoandaliwa ili kukidhi jambo hili ndani na nje ya vyumba vya habari... Ninatumaini litasaidia kushughulikia changamoto tunazopambana nazo leo."*

Ingawa kwa kiasi fulani anakubaliana na mtazamo huu, mhojiwa kutoka vyuo vya uandishi wa habari, anajenga hoja kuwa kama wahitimu wengine, wahitimu wa uandishi wa habari ni zao la mfumo ule ule. Kwake, tatizo hili ni kubwa na haliwezi kutatuliwa na taasisi za elimu pekee. "Sisi [vyuo vikuu] tunapokea wanafunzi ambao tayari wana mapengo, na inahitajika juhudi za ziada kwa pande zote [wanafunzi na wakufunzi] kuziba mapengo haya. Wanafunzi wanahitaji kuandaliwa vema tangu shule za msingi."

Hata hivyo, mhojiwa aliongeza kuwa kwa programu za masomo zenye vitendo zaidi kama uandishi wa habari, taasisi za mafunzo zinapaswa zihakikishe kuna uwiano kati ya nadharia na vitendo. Jambo hili linajumuisha kuajiri wakufunzi zaidi watakaoshughulikia kozi za vitendo kwa sababu wakufunzi wengi wa sasa hawajafanya kazi ya uandishi wa habari na hivyo kuwa ngumu kufundisha fani hii.

Changamoto za kiuchumi zimejazimisha vyombo vya habari kadhaa kupunguza idadi ya wafanyakazi. Leo, vyumba vya habari vina waandishi wachache, wahariri wasaidizi,

watangazaji na wazalishaji vipindi wachache, na hata wasomaji hakikifu wachache sana au pengine hakuna kabisa. Hawa wanatarajiwa kufanya kazi katika majukumu yale yale. Jambo hili linaibana sana nguvukazi iliyobakia.

## 6.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulitathmini ubora wa uripoti wa vyombo vya habari nchini Tanzania. Ulitumia uchambuzi wa maudhui na viashiria mahususi vya ubora.

Matokeo yanaonesha kuwa ubora wa uripoti kwa mwaka 2019, kwa jumla, uliporomoka ukilinganisha na matokeo ya mwaka 2018. Hata hivyo, kuna tofauti za msingi kati ya aina ya vyombo vya habari na vyumba vya habari. Kwa jumla, waandishi wa habari wameongeza idadi ya habari za kutafuta wenyewe kwa asilimia 2, huku vipindi vya redio vikiboreshwa kwa asilimia 9, na magazeti yakiporomoka kwa asilimia 6. Matumizi ya vyanzo mbalimbali vya habari kwa jumla yameshuka kwa asilimia 5 katika habari za redio, katika vipindi vya televisheni na magazeti yameporomoka kwa asilimia 11 na 9 mtawalia. Ujumuishwaji wa mitazamo katika habari na vipindi umeshuka katika majukwaa yote ya vyombo vya habari.

Tofauti baina ya aina za vyombo vya habari na baina ya vyumba vya habari zimebainika wazi. Magazeti bado yanafanya vizuri katika vigezo vingi yakiwa na kielezo cha ubora wa asilimia 27.4, yakifuatiwa na vituo vya televisheni (asilimia 26.9), redio za mikoani (asilimia 26.1), na redio za kitaifa (asilimia 25.5). Utoaji wa viwango katika kielezo cha ubora unaonyesha kuwa vyombo vya habari vitano vilivyofanya vizuri ni Micheweni FM (asilimia 41), Radio One, Raia Mwema, na Mwananchi (kila moja ikiwa na asilimia 36), na Jamhuri (asilimia 34). Vyombo ambavyo havikufanya vizuri ni ZBC TV, Clouds FM, TBC1 na Habari Leo (kila moja ikiwa na asilimia 25), TBC Taifa na The Guardian (kila moja ikiwa na asilimia 23), na Ayo TV (asilimia 5).

Matokeo pia yanaonyesha kuwa redio za mikoani zilizipiku redio za kitaifa katika viashiria vingi vya ubora, jambo linalosisitiza hitaji la kuwekeza zaidi katika vituo vya redio mahususi za mikoani nchini. Aidha, kama ilivyokuwa mwaka 2018, vyombo vya habari vya Zanzibar vinachuana vema na vyombo vya habari vilivyoko Tanzania bara.

Kwa kuzingatia matokeo haya, utafiti

unapendekeza hatua kadhaa kwa wadau tofauti wa habari kama vile vyombo vya habari, mashirika ya habari, wadau wa maendeleo, serikali na taasisi za mafunzo ya uandishi wa habari.

### **5.1 Mapendekezo kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari**

Vyombo vya habari vinahitaji kufanya maboresho katika vipengele vingi, hususani katika upana wa uripoti wa habari. Kwa mfano, vinapaswa kuripoti habari katika mitazamo mbalimbali, kuongeza usuli wa kihistoria kwa habari, kuongeza idadi ya vyanzo vya habari, na kuboresha mizania katika kutoa misimamo kinzani.

Vyombo vya habari vinashauriwa kushirikiana na wakufunzi maalumu ambao wameandaliwa kupitia utafiti huu na wanaotoka kwenye vyumba mbalimbali vya habari nchini. Wakufunzi hawa walipatiwa mafunzo kuhusu vigezo vya ubora vinavyotumika kwenye utafiti huu, na hivyo kuwa rahisi kwao kufundisha kwa kutumia vigezo hivyo.

Kwa lengo la kuboresha ubora wa habari, vyombo vya habari vinashauriwa kuandaa mafunzo ya ndani kwa kuzingatia changamoto za utoaji wa habari au mapengo yaliyobainishwa katika utafiti huu na kielezo maalumu cha ubora wa chombo husika cha habari.

Kutokana na hali ya kiuchumi iliyopo, inapendekezwa vyombo vya habari vianze kufikiria njia mbadala ambazo zitasaidia kupanua vyanzo vyao vya mapato, na sio kutegemea matangazo pekee.

### **5.2 Mapendekezo kwa mashirika yanayosaidia vyombo vya habari**

Kuna mashirika kadhaa nchini yanayofanya kazi za kuimarisha ubora wa uripoti wa vyombo vya habari. Mashirika haya yanashauriwa kuandaa programu zao za ubora wa uripoti wa vyombo vya habari katika namna ambayo inashughulikia changamoto zilizobainishwa katika ripoti hii. Mashirika haya yanaweza kujumuisha vigezo vya ubora vilivyotumiwa katika utafiti huu katika kuandaa programu zao. Kwa kufanya hivi kunaweza kusaidia kushughulikia changamoto za uripoti wa habari zilizobainishwa kwenye utafiti huu. Pia, wanashauriwa kutumia wakufunzi

maalumu walioandaliwa chini ya utafiti huu kwenye programu zao.

### **5.3 Mapendekezo kwa wadau wa maendeleo**

Wadau wa maendeleo wanakaribishwa kuangalia matokeo ya utafiti huu kwa ajili ya jitihada zao mbalimbali za kuboresha mazingira ya habari nchini. Pia matokeo ya utafiti huu yanaweza kuwa chanzo cha ushauri katika masuala mahsusi kwa wadau wanaofanya kazi pamoja na vyombo vya habari.

Kwa kuwa lengo la jitihada hizi ni kusaidia kuimarisha ubora wa vyombo vya habari nchini, inapendekezwa kuwa wadau wa maendeleo washiriki katika mkakati huu ama kama ulivyo sasa au vinginevyo kama vile kuunga mkono utafiti maalumu ambao unalenga, kwa mfano, uripoti wa vyombo vya habari kwenye masuala ya maendeleo, fedha na uchumi, siasa n.k.

### **5.4 Mapendekezo kwa Serikali**

Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 imependekeza uanzishwaji wa Mfuko wa Mafunzo kwa Vyombo vya Habari ambao malengo yake, pamoja na mambo mengine, ni kuwezesha mafunzo kwa wanahabari. Ingawa Mfuko huu bado haujaanzishwa, matokeo ya utafiti huu yanaweza msingi ambao Mfuko huo pindi utakapoanzishwa utapata sehemu ya kuanzia.

Ili kutatua hali ya sasa ya kujidhibiti kuandika baadhi ya habari kwa wanahabari inayohusishwa na mazingira ya sasa ya kisiasa, ripoti hii inapendekeza kuwa serikali na wadau wa vyombo vya habari kwa pamoja washirikiane kutatua changamoto hizi kupitia meza ya majadiliano.

### **5.5 Mapendekezo kwa taasisi za mafunzo**

Kwa taasisi zinazotoa mafunzo kwa waandishi wa habari, inapendekezwa zijumuishe vigezo vya ubora vya uripoti vilivyotumika katika utafiti huu katika mitaala yao. Kwa kuzingatia uhaba wa machapisho stahiki na ya ndani na tafiti kuhusu ubora wa uripoti wa vyombo vya habari nchini, taasisi hizi zinapaswa kufikiria kuongeza ripoti hii katika marejeleo yao ya kitaaluma.

## VIAMBATISHO

### Faharasa

ISTILAH	UFAFANUZI
Mada kuu katika habari	Inatathminiwa kutokana na orodha ya mada 38, yaani habari inahusu mada ipi.
Habari za mijini na nje ya miji	Inachunguzwa iwapo makala inahusu masuala au matukio yanayotokea katika miji mikubwa ya Tanzania bara na Zanzibar (Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya, Mjini Magharibi na Kusini Pemba) au miji midogo na maeneo ya vijijini.
Kulenga mikoani	Inachunguzwa kujua habari inatoka katika wilaya ipi ya Bara au Zanzibar.
Habari ya kitaifa au ya eneo fulani	Inatathminiwa kwa kuzingatia iwapo habari inaeleza suala pana la kitaifa au suala linahusu eneo fulani pekee.
Muktadha wa upatikanaji habari	Inatathminiwa kama habari husika ni zao la habari za kimatukio au ni ya kutafutwa na waandishi wa habari wenyewe.
Idadi ya vyanzo vya habari	Inatathminiwa kwa kuzingatia vyanzo vingapi vya habari vilivyotajwa kwenye kazi moja ya kiuandishi.
Idadi ya wanawake kama vyanzo vya habari	Inatathminiwa idadai ya wanawake ambao ni vyanzo vya habari.
Mitazamo ndani ya habari	Inatathminiwa mada inawasilishwa katika mtazamo upi (sera, siasa, uchumi, masuala ya kawaida, usalama), na kama habari ina mtazamo mmoja au zaidi.
Mtiririko dhahiri wa habari	Inatathminiwa kama kazi ya habari ina mtiririko thabiti au dhaifu wa kiuandishi.
Usuli / historia	Kigezo hiki kinatazama kama kazi ya habari imebeba usuli wa kihistoria wa habari husika, na kwa kiwango gani (aya ngapi).
Kiini/mzizi wa habari	Hili linatathminiwa kwa kuangalia iwapo kazi ya kihabari inafafanua viini vya tatizo au suala husika. Viini vinavyorejelea tatizo katika habari ndivyo pekee vinavyotathminiwa.
Maoni ndani ya habari	Kigezo hiki kinatazama maoni yanayotolewa na vyanzo vya habari kama ni maoni kamilifu au ni maneno ya juu juu.

ISTILAH	UFAFANUZI
Maoni kinzani	Kigezo hiki kinapima ni kwa kiasi gani habari imebeba maoni yanayokizana. Hii inawezesha kuwa na uhakika wa tafakuri yenye mizania kuhusu suala linaloelezwa.
Haki ya kujibu tuhuma	Inatathiminiwa kama habari inatoa haki ya kujibu tuhuma kwa wale wanatuhumiwa kwenye habari husika, isipokuwa habari zinazohusu jinai na kesi zilizoko mahakamani.
Uwekaji wa takwimu kwenye muktadha	Kigezo hiki kinatazama kama takwimu zilizotumika kwenye habari zimefafanuliwa vizuri kwa kuziweka katika muktadha, yaani kuzilinganisha na kitu fulani ambacho msomaji au msikilizaji anakielewa vizuri.
Muundo wa kiuandishi	Kazi ya kihabari lazima iwiane au iwe na mtiririko ili hadhira iielewe kwa urahisi. Kwa hiyo, inapaswa kuwa na uhusiano dhahiri na wa kimantiki ili sehemu mbalimbali za habari hiyo ziwe na upatanifu. Hili linatazamwa pia.

## Vigezo vya Kielezo cha Ubora wa Vyombo vya Habari

- **Muktadha wa upatikanaji habari:** % ya habari ambazo zilitokana na jitihada binafsi za vyombo vya habari. Si habari za matukio.
- **Vyanzo vingi vya habari:** % ya habari zilizotumia vyanzo viwili au zaidi.
- **Idadi ya mitazamo katika habari:** % ya habari zilizokuwa na angalau mitazamo miwili.
- **Idadi ya maoni ndani ya habari:** % ya habari zilizotumia walau maoni 2 au maoni ya watu wawili.
- **Uelezeaji wa kiini/mzizi wa habari (root causes):** % ya habari zilizotumia walau aya mbili (katika magazeti) au sentensi mbili (katika redio na televisheni) kuelezea kiini/mzizi wa habari kuu.
- **Usuli kwenye habari:** % ya habari zilizotumia aya mbili (katika magazeti) au sentensi mbili (katika redio na televisheni) kutoa usuli wa habari kuu.
- **Muundo wa kiuandishi:** % ya habari ambazo zilikuwa na muundo mzuri sana, aya na vipengele mbalimbali vya matini vilivyoshikamana vizuri.
- **Haki ya kujibu tuhuma:** % ya habari zilizotoa nafasi ya haki ya kujibu tuhuma kwa watuhumiwa.
- **Habari zenye kumulika serikali:** % ya habari ambazo zilikuwa na maoni au mitazamo iliyokuwa inakosoa serikali.
- **Matumizi ya takwimu katika muktadha:** % ya habari ambazo kwa kiasi kikubwa ziliweka takwimu katika muktadha mzuri.



Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na  
Mawasiliano kwa Umma  
S.L.P 4067 Mikocheni B  
Makaburi Street, Plot Block D, No.34  
Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255 22 2700756  
Barua pepe: [sjmc@udsm.ac.tz](mailto:sjmc@udsm.ac.tz)  
Tovuti: [www.udsm.ac.tz](http://www.udsm.ac.tz)



Schweizerische Eidgenossenschaft  
Confédération suisse  
Confederazione Svizzera  
Confederaziun svizra

**Embassy of Switzerland in Tanzania**

